epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Nipashe

Jumamosi Julai 20, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581743

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMI

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA WA 2
**Wananchi** wafikisha kilio athari za tuta SGR



UKURASA WA 5
**Wamwangukia** Waziri Silaa uvamizi ardhi

UKURASA WA 5
**Walimu** 10 wafundisha wanafunzi 800

UKURASA 22
**ENGLAND YAMSUBIRIA GUARDIOLA MBADALA WA SOUTHGATE**

RIPOTI MAALUM

# Taifa linaangamia

• **Kamari** karibu kila nyumba, shisha hadi kwenye makazi...*Endelea ukurasa 4*



Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu (kulia), akizungumza na Makamu wa Rais wa Chama kikuu cha upinzani nchini Malawi cha Democratic Progressive Party (DPP) Dk. George Chaponda (mwenye suti ya bluu), alipotembelea ofisi za chama hicho, jijini Dar es Saam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## ACT yapewa mbinu za kushinda uchaguzi

UKURASA 3



## Makonda adaiwa kukiuka sheria, haki za binadamu

UKURASA 2

**MICHEZO** **GAMONDI: NGUVU ZETU KWENYE UBINGWA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Wafikisha kilio haki za binadamu tuta SGR

**Na Idda Mushi,**
MOROGORO

WAKAZI wa eneo la Block Five, Kata ya Kihonda, Manispaa ya Morogoro, wamewasilisha malalamiko Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuhusu athari mbalimbali walizozipata baada kujengwa kwa tuta la reli ya kisasa (SGR) ikiwamo kuingilika kwa njia moja ambayo wakati wa mvua hugeuka mto kupitisha maji, hivyo kushindwa kutumika na watu.

Baadhi ya wananchi hao, Yesse Mnzava, Joseph Msofe, Grace Chilongola, Edwin Claver, Juma Tegeje, Abel Isaya ambaye ni mwakilishi wa mwekezaji wa kiwanda cha Kuku, licha ya kupongeza uwepo wa SGR kurahisisha huduma za usafiri kwa haraka, alisema ujio huo pia umesababisha matatizo makubwa kwa wakazi ikiwamo gharama kubwa za maisha.

Walisema hayo baada ya ujumbe wa timu ya wataalamu wa tume hiyo kufika eneo hilo kwa lengo la kukusanya maoni ili kuandaa mpango mkakati wa miaka mitano wa kitaifa kuhusu haki za binadamu na biashara.

Kutokana na kuwapo kwa tuta hilo, waliiomba serikali kuwajengea kivuko cha juu (flyover) ili kurahisisha watu kuingia na kutoka katika eneo hilo wakati wote.

Mnzava alisema mradi huo wa SGR ulisahau kuweka miundombinu rafiki kwa wananchi hasa barabara za kuingia na kutoka na kubakiza njia moja tu kwenye mkondo wa maji, hivyo kusababisha kipindi cha mvua watu kushindwa kuitumia kutokana na kupitisha maji.

Pia alisema njia hiyo moja kwa umbali mrefu imeongeza gharama kubwa za maisha na wanafunzi kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilometa 10 ili kufikia njia ya kutoka, huku wale wa Shule ya Sekondari ya Uluguru waliokuwa wakitumia kati ya nusu kilometa na kilometa mbili, kutumia umbali huo.

Mnzava alisema serikali haikutilia maanani mahitaji ya wananchi wakati wa utekelezaji wa mradi huo kwa kuwa haikuzingatia mahitaji ya wananchi na taasisi zilizoko zikiwamo shule namna watakavyopata huduma.

Naye chilongola alisema huduma mbalimbali kama hospitali, zahanati na kituo cha polisi hazipatokani na ikitokea mgonjwa anahitaji huduma ya dharura au haraka, inakuwa vigumu jambo ambalo linaweza kusababisha kupoteza maisha hasa nyakati za mvua.

Isaya kwa upande wake alisema kwa sasa wamekuwa na wakati mgumu kutoa huduma kutokana na miundombinu isiyo rafiki, huku mageti kwenye barabara ya akiba ya reli waliyokuwa wakiitegemea yakifungwa na kuzuia magari kupita.

Pia alisema ubovu na kujaa maji kwa barabara kumesababisha mizigo yao kuharibia na kuna wakati gari lenye mzigo wa mayai lilipinduka na kuwasababishia hasara ya zaidi ya Sh. milioni tano

"Sasa tumekuwa tukijiendesha kwa hasara. Hakuna mwekezaji anataka kuwekeza kwenye eneo kwenye changamoto ya miundombinu, iwe barabara, maji au umeme na wakati wowote anaweza kufunga biashara yake na kusababisha watu kukosa ajira. Hata kile alichokuwa akisaidia jamii kupitia ujirani mwema watakikosa," alisema huku akibainisha kuwa kiwanda hicho ni miongoni mwa wawekezaji wakubwa katika ulipaji wa kodi kwa Morogoro. Wananchi hao pia wliashangazwa na mkandarasi aliyekuwa akichukua kifusi katika maeneo hayo, kushindwa kurejesha vyema mazingira kama sheria inavyotaka kwa kuacha shimo kubwa hadi sasa kwenye eneo la makazi ambalo limeendelea kujaa maji na kuwa tishio kwa kuwapo mazalia ya mbu pamoja na kichaka kikubwa kinachoweza kutumika kuficha wahalifu.

Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Nabo Assey, aliahidi kupeleka malalamiko hayo na kuyafanyia kazi ikiwapo kuyafikisha kwenye wizara za kisekta.

Assey alisema kilichoonekana katika maeneo hayo ni mamlaka za serikali kukosa mawasiliano wakati wa utetelezaj wa miradi na kwamba anaamini mpango kazi huo utatoa suluhu ya tatizo hilo. Mwenyekiti wa Mtaa wa Yespa, Rukia Gunda, licha ya kushukuru kuwapo kwa reli hiy ya kisasa, alisema ukosefu wa vivuko umesababisha wananchi kutembea kwa miguu umbali mrefu na kuchelewa kazini na shuleni huku wengine wakilazimika kutumia pikipiki au baiskeli kwenda kazini.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akipokea kutoka kwa Mwenyekiti wa Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Pentekoste Tanzania (CPCT), Dk. Barnabas Mtokambali vitendea kazi vya baraza hilo, ikiwemo Dira ya Maendeleo, wakati wa kilele cha Mkutano wa Baraza hilo, Miyuji jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Makonda adaiwa kukiuka haki za binadamu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imetoa matokeo ya uchunguzi wa malalamiko yanayohusu uvunjwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya utawala bora kuhusu viongozi kadhaa, akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda.

Uchunguzi huo umehusisha malalamiko 14 ikiwamo dhidi ya Makonda, aliyelalamikiwa kutoa amri ya kukamatwa na kuwekwa mahabusu mkazi wa mkoani humo kinyume cha utaratibu na sheria Juni, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu, akitoa taarifa ya uchunguzi wa malalamiko hayo kwa waandishi wa habari jana jijini hapa, alisema malalamiko 14 yaliyowasilishwa yamefanyiwa uchunguzi.

Alisema katika uchunguzi dhidi ya Makonda, THBUB imebaini kuwa amri iliyotolewa haikuwa halali na haikuzingatia aina ya makosa na utaratibu unaoainishwa kisheria wa utekelezaji wa mamlaka hayo.

"Na kwamba mwananchi huyo hakuwa mhusika wa madai ya msingi ambayo mkuu wa mkoa huyo aliyatumia kushughulikia suala lililokuwa mbele yake.

"THBUB imebainika kuwa pia, Makonda alivuka mipaka ya majukumu yake kwa kushughulikia na kutoa uamuzi katika suala ambalo lilipaswa kufuata mkondo wa kisheria wa kimahakama kwa kuwa madai hayo yangeshughulikiwa huko," alisema.

Jaji Mstaafu Mwaimu alisema hata kama kulikuwa na viashiria vya makosa ya jinai, njia sahihi ingekuwa kulielekeza Jeshi la Polisi kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

"THBUB pia ilibaini kutozingatiwa kwa haki za mtuhumiwa kwa kuwekwa mahabusu kwa saa 96 (yaani siku nne) bila kufunguliwa mashtaka," alisema Jaji Mwaimu

Kadhalika alisema pamoja na mkuu huyo wa mkoa kuitwa mbele ya THBUB ili kuwasilisha utetezi wake alikaidi kufanya hivyo.

**GEKUL**

Mwenyekiti huyo alisema tukio lingine lililofanyiwa uchunguzi ni lile la aliyekuwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul, aliyehusishwa na kuwaingiza chupa sehemu ya haja kubwa, Hashim Ally na Michael Isara.

Alisema baada ya uchunguzi kwa kuzingatia maelezo ya watu mbalimbali waliohojiwa na vielelezo ambavyo THBUB ilivipata haikubaini suala hilo kufanyika.

"THBUB ilibaini kuwa walalamikaji walizuiliwa kwa muda mrefu wakati wakihojiwa na mlalamikiwa kuhusu tuhuma za kutaka kumwekea sumu Pauline Gekul pamoja na kupeleka madawa ya kishirikina katika hoteli yake iitwayo Paleii Lake View na hivyo kusababisha walalamikaji kukosa haki yao ya kuwa huru" alisema.

Hata hivyo, alisema taarifa za uchunguzi zenye mapendekezo kwa kila uchunguzi uliofanyika zimewasilishwa katika mamlaka husika kwa ajili ya utekelezaji.

## HABARI KITAIFA

# ACT yapewa mbinu kushinda uchaguzi

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimepewa mbinu za kushinda uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani ikiwamo kutoruhusu migogoro na migongano ya ndani inayosababisha vyama kupoteza lengo.

Makamu wa Rais wa Chama Kikuu cha Upinzani cha Democratic Progressive (DPP) cha Malawi, Dk. George Chaponda, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumza na viongozi wa ACT Wazalendo.

Dk. Chaponda alisema migogoro ya ndani ya chama haina afya na imekuwa ikisambaratisha vyama vya siasa.

"Chama chetu kilipotolewa madarakani tulijikuta tukiwa chama cha upinzani. Siri ya kushinda uchaguzi ni kubeba ajenda za umma," alisema.

Dk. Chaponda alisema chama kinatakiwa kubeba ajenda za umma bila kuchoka na kuachana na mlolongo wa ajenda zinazoweza kuwapoteza wananchi na kushindwa kuwaelewa viongozi wa chama wanataka nini.

Alisema chama chake kimejifunza jambo kutoka Chama cha ACT Wazalendo, kwa jinsi kinavyozingatia usawa wa kijinsia katika uongozi.

Kiongozi wa ACT Wazalendo, Dorothy Semu, alisema ACT Wazalendo kimeendelea kusimamia utawala bora unaoheshimu misingi ya kidemokrasia na kinatekeleza hayo kwa vitendo.

"Chama kimeendelea kuwapa nafasi za uongozi vijana na wanawake, tuna ngome ya vijana na wanawake kuanzia taifa hadi kijiji," alisisitiza.

Kuhusu demokrasia katika nchi za Afrika, Semu alisema bado kuna vikwazo katika uchaguzi, huku akiomba kudumisha ushirikiano na namna bora ya kuviondoa.

Alisema Julai 22, mwaka huu, chama hicho kinajiandaa kuzindua programu maalum ya kusajili wanachama milioni 10 kwa miezi 10, ikiwa ni sehemu ya kuimarisha mtandao wa chama kujiandaa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

# PM asisitiza ushirikiano dini, serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani), amezitaka taasisi za dini nchini kuendelea kushirikiana na serikali kutoa mchango kwenye maendeleo ya taifa.

Amesema kuwa taasisi za dini zina uwezo mkubwa wa kutoa huduma imara za kiroho na kugusa maisha ya watu katika jamii na kuwaletea maendeleo ya kiuchumi na kisiasa.

Majaliwa alitoa wito huo jana kwenye Kilele cha Mkutano wa Baraza la Maaskofu wa Makanisa ya Pentekoste Tanzania (CPCT), uliofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Biblia Miyuji, jijini Dodoma.

"Tuna kila sababu ya kuyashukuru makanisa kwa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo ya wananchi kwa ujumla, yamekuwa sehemu ya suluhisho katika changamoto za kijamii kama vile umaskini, elimu duni, na matatizo ya kiafya.

"Nitumie fursa hii kusisitiza taasisi za dini kuendelea kuimarisha ushirikiano na serikali na kuendelea kuiishi kwa vitendo kaulimbiu yenu ya Palipo na Umoja, Bwana Huamuru Baraka! Bwana Huamuru Baraka Palipo na Umoja," alisema.

Katika hatua nyingine, Majaliwa alisema serikali inathamini mchango wa taasisi za dini katika kuhubiri amani na utulivu nchini.

"Siri ni ya haya yote ni sababu ya uwapo wa dini katika kuhubiri maadili, mshikamano, upendo uvumilivu na kuwa wamoja, serikali pekee tusingeweza," alisema.

Mwenyekiti wa CPCT, Askofu Dk. Barnabas Mtokambali, alisema baraza hilo kupitia madhehebu wanachama wake, litaendelea kushirikiana na serikali katika kuendeleza sekta za elimu, na afya nchini kwa kujenga na kuendesha hospitali, vituo vya afya, shule na vyuo vya aina mbalimbali.

"Hili si tu kwamba linapunguza mzigo mkubwa wa serikali katika kuihudumia jamii kubwa ya Watanzania katika mahitaji husika, bali pia linasaidia kupunguza tatizo kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana," alisema.

Aliongeza kuwa CPCT itaendelea kushirikiana na serikali katika kuhimiza maadili mema kwa mafundisho ili kupinga wimbi la mmomonyoko wa maadili linaloukumba ulimwengu mzima.



"Baraza limekuwa mstari wa mbele kupinga vitendo kama ndoa za jinsia moja, ushoga, kutokuwajibika kwa wazazi kutunza familia kunakosababisha kuongezeka kwa watoto wa mitaani, mila potofu za ukeketaji wanawake, imani za kishirikina zinazopelekea watu wenye ulemavu wa ualbino kuuawa kwa dhana," alisisitiza.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Taifa linaangamia

## -Kamari karibu kila nyumba, shisha katika makazi

**Na Romana Mallya**



TAIFA linaangamia, kilio kinasikika kwa wazazi; karibu kila mtaa kuna mashine ya kamari (dubwi) ambao walengwa wakuu ni watoto na vijana - taifa la kesho na kilevi aina ya shisha kimesogezwa hadi kwenye makazi ya watu.

Ni kadhia iliyoenea katika miji mikubwa nchini ingawa kamari kwa watoto sasa inaripotiwa hadi vijijini huku Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikiagiza mamlaka husika kushughulikia kero za wananchi zikiwamo hizo kisha taarifa kamili waikabidhi.

Katika eneo la Mwananyamala Kisiwani, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, kwa mfano . imebainika kamari kwa watoto na vijana umri wa kwenda shuleni hivi sasa si msamiati mpya; wenyeji wanalalamika karibu kila baada ya nyumba kadhaa kuna mashine za mchezo huo.

Uchezaji kamari kwa watoto ni kinyume cha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya Mwaka 2003, Kifungu 70 kinachokataza watoto kucheza kamari. Vitendo hivyo pia vinakinzana na Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ya Mwaka 2009 inayoelekeza wazazi/walezi, jamii na serikali kuhakikisha mtoto analindwa dhidi ya vitendo viovu vikiwamo kamari na ukatili.

Wakazi wa Mwananyamala pia wanalalamika kwamba makazi hayo kwa sasa yana shinda nyingine - shisha ambayo awali maskani yake yalikuwa katika kumbi za starehe kwa matajiri (Cassino).

Wanasema hivi sasa kilevi hicho kinapatikana kwa bei rahisi (inahifadhiwa) katika makazi ya watu hasa maduka madogo ya pombe na kuchangia wengi kutumbukia kuvuta.

Mmoja wa wanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Msimbazi (jina linahifadhiwa kwa sababu ni mtoto) ambaye ni mkazi wa Mwananyamala, ameiomba serikali ifanye kila inaloweza kuondoa kamari mitaani pamoja na shisha kwa sababu zimekuwa zikiathiri watoto na vijana na baadhi badala ya kwenda shule wanashinda huko.

"Kwa ujumla hali ni mbaya. Watoto na vijana wenzetu wanaharibika, wanapotoka kimaadili. Jeshi la Polisi na mamlaka zingine husika ziendelee kukomesha haya hasa huku mitaani.

"Vitu hivi vinapoendelea kuwapo huku mtaani vinachangia mmomonyoko wa maadili kwa watoto na vijana ni rahisi kurubunika. Mtoto anapewa fedha za matumizi ya shuleni lakini zinaishia huko na wengine wanajiingiza katika udokozi mdogo mdogo ili tu kupata fedha za kucheza kamari au kuvuta shisha," anasema.

Shambani Chamulume, mkazi wa Buguruni, Ilala jijini Dar es Salaam, ameomba serikali iongeze nguvu ya mapambano ya matatizo hayo.

"Ninaamini serikali haiwezi kushindwa kukomesha michezo ya kamari au shisha katika makazi ya watu nchini endapo itaamua.

Wazazi tuna hali ngumu katika malezi ya watoto wetu wamezungukwa na vishawishi vibaya.

"Tunajitahidi kadri tuwezavyo, lakini mtoto leo akienda mtaani kucheza anakutana na ushawishi wa kamari na shisha au dawa za kulevya, mambo haya wakuyakomesha ni serikali kwa kushirikiana na wananchi, tunaomba nguvu iongezwe," anasema.

Monica Kilawe, mkazi wa Mtaa wa Mchangani, Kata ya Mwananyamala, mkoani Dar es Salaam, anasema kero ya watoto hao ipo pia, stendi ya daladala ya Makumbusho ambako kuna watoto wanavuta bangi, shisha na kucheza kamari.

"Ninachokiona sisi wazazi ni kama hatuwafuatilii watoto wetu, tukishawasukuma shuleni basi, nyumbani wakija karibu mwanangu njoo ule akishashiba humwambii kaa hapa soma, anakwenda mtaani kuzurura.

"Hata akitoka humuulizi kaenda wapi na akirudi humuulizi katoka wapi? Wazazi tuwaangalie sana watoto. Kuna ugumu katika kulea mtoto katika mazingira haya tunaishi huku kwa kuwa tumejenga.

"Ukweli ni kwamba kila baada ya nyumba kadhaa utakuta shisha au dawa nyingine za kulevya zinauzwa au michezo ya kamari. Tunaomba wale wanaohusika kuuza michezo ya kamari au shisha watambue huu ni uuaji wa taifa la kesho na watambue wanaliangamiza taifa Tanzania," anasema.

**WILAYA IKO MACHO**

Mkuu wa Wilaya wa Kinondoni, Saad Mtambule, anasema wilaya hiyo haijakaa kimya inaendelea kuchukua hatua kwa kushirikiana na wadau wa haki jinai na viongozi wa dini.

"Tumetengeneza kamati mahsusi ya kuendelea kuhamasisha katika maeneo mbalimbali, kwenye makanisa na misikiti na mitaa yetu.

"Kila mmoja apaze sauti juu ya mmomonyoko wa maadili ikiwamo matumizi ya dawa za kulevya, ulawiti, ubakaji, ushoga, kujiuza kwenye mitaa, uzururaji na wizi haya yote tunaendelea kuyasukuma.

Aidha, kiongozi huyo akaomba wananchi kubeba jukumu la kupinga vitendo hivyo kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa akihamasisha jamii kufuatilia mwenendo ya watoto na malezi yaliyobora kulingana na mila na desturi, tamaduni za kitanzania.

Diwani wa Makumbusho, Mohamed Ali, amekiri kuwapo kwa kamari katika makazi ya wananchi.

"Suala hili tumekuwa tukilifanyia kazi, lakini mara nyingi kuna wale anaotoa leseni za biashara hizi ndio wanaotuletea uzito.

"Lakini tumeshapeleka suala hili mamlaka husika, ninafikiri leseni zao zinaangalia wapi biashara hii inakwenda kufanyika. Kadhalika sehemu za kuvutia shisha wengine wanavuta vijiweni, hili tumewaachia vyombo vya ulinzi na usalama kulishughulikia," anasema.

Akizungumzia hali kwa ujumla katika maeneo hayo, Ali anasema awali maeneo mengi yalikuwa yameharibika kwa uvutaji wa dawa za kulevya.

"Kama ulisikia sheria iliyotoka juzi hapa kuna baadhi ya wauzaji wa dawa za kulevya wamepata vifungo vya maisha, kuna watu wengine walioko katika mitaa yetu baada ya hukumu ile kutolewa wamehamasika kuacha biashara hii kwa maana kwamba, wanajua watakapokamatwa hukumu nzito itawakuta," anasema.

**MAAGIZO CCM**

CCM haiko mbali na kinachojiri Mwananyamala na maeneo mengine nchini, hivyo Katibu Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, ameagiza kabla hajamaliza ziara katika mkoa wa Dar es Salaam, Mkuu wa Wilaya hiyo na timu yake waandae majibu ya kero za wananchi zikiwamo hizo ambazo wananchi wamezilalamikia.

"Na mengine waliyosema yatembeleeni, fikeni muone, kila lililosemwa mjiridhishe mwende katika maeneo hayo. Mpaka ninamaliza ziara nipate kalabrasha lililokamilika kila mwananchi amepata majibu yake," aliagiza.

ITAENDELEA KESHO

# Wamwangukia Silaa uvamizi maeneo

**Na Samson Chacha,** TARIME

BAADHI ya wakazi wa Tarime mkoani Mara, wamemwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, kufika wilayani humo kuingilia kati migogoro ya ardhi.

Migogoro hiyo inadaiwa kutokea kutokana na ubadilishwaji wa michoro ya ramani kutoka kuwa maeneo ya miradi ya kimaendeleo na kufanywa makazi ya watu.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hii kwa nyakati tofauti, wananchi hao walimwomba waziri huyo afike wilayani hapa ili watoe malalamiko na kero zao kutokana na uvamizi uliopo.

"Maeneo hayo ni pamoja na ya miradi ya viwanja vya michezo, ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari, hifadhi za barabara, stendi ya magari sirari ambayo yamebadilishwa michoro ya ramani.

"Wamebadilisha kuwa maeneo ya makazi, mashamba na kuchangia migogoro mingi ya ardhi na ukosefu wa maeneo ya kutekeleza miradi hiyo," alisema Ally Mrimi, mkazi wa mji wa Nyamwaga.

Matiko Nyandira, mkazi mwingine wa mji wa Sirari, alisema mwanzoni mwa mwaka huu, ilifanyika kliniki ya ardhi ambayo iliongozwa na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, na Mkuu wa Wilaya wakati huo, Kanali Michael Mtenjele.

Wengine walikuwa Kamishna wa Ardhi

Msaidizi Mkoa, Baraka Kambiri. Licha ya kero hizo kuibuliwa na kuahidiwa kufanyiwa kazi, hadi sasa hawajaona utekelezaji wake.

"Mbali na kliniki hiyo ya ardhi kupokea malalamiko yetu kuhusu migogoro ya ardhi iliyopo hapa, bado hatua za kisheria hazijachukuliwa kuwaondoa wavamizi wa maeneo hayo, huku watu wakiendeleza ujenzi wakidai kupewa vibali na maofisa ardhi," alisema Nyandira.

Charles Maguge, mkazi wa Tarime Mjini, alisema ujenzi huo umesababisha kuzibwa kwa barabara na mitaa kutokupitika kwa ajili ya huduma muhimu na za dharura.

Akijibu madai hayo, Ofisa Ardhi wa Wilaya ya Tarime, Philipo Mracha, alikiri kupokea kero nyingi kuhusu migogoro ya ardhi na sasa wanaendelea kuzifanyia kazi ili kuhakikisha wanazipatia ufumbuzi wa haraka.

Pia alikiri kuwapo kwa baadhi ya watumishi katika ofisi hizo ambao siyo waadilifu wanaosababisha kutokea kwa migogoro hiyo, huku akibainisha kwamba uchunguzi dhidi yao unaendelea.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Kanali Maulid Surumbu, alisema tayari malalamiko hayo yamepokewa serikalini na kutaka wananchi hao kuwa na subira wakati yakifuatiliwa ili kutatua kero hizo.



Mshtakiwa Samwel Gombo, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kuhukumiwa kifungo cha miaka mitano jela katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam juzi, kwa makosa ya kughushi nyaraka na wizi wa zaidi ya milioni 102 za marehemu. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Walimu 10 wafundisha wanafunzi 800

**Na Mary Mosha,** MWANGA

WANAFUNZI 800 wa shule za awali na msingi tatu katika kata ya Kigonigoni, Mwanga mkoani Kilimanjaro, wanafundishwa na walimu 10, wawili kati yao wako likizo ya uzazi na mmoja alifariki dunia wiki iliyopita kwa kujinyonga.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wazazi akiwamo Omary Iddy, walisema katika kata hiyo kuna shule za msingi tatu ambazo kuna uhaba mkubwa wa walimu.

"Shule zilizopo ni Kigonigoni yenye wanafunzi zaidi ya 410 na ina walimu sita ambapo mmoja anapaswa kuhama kwenda Kagera. Shule ya Kwakihindi ina wanafunzi takribani 200 na walimu wanne, wawili kati yao wako kwenye likizo ya uzazi, hivyo waliopo ni wawili tu.

Vilevile shule ya Kwa Ruru ina wanafunzi takribani 200 na walimu wanne ambapo mmoja kati yao alijinyonga wiki iliyopita (mkuu wa Shule) kwa sababu ya matatizo ya kifamilia,"alisema.

Abdtway Kajiru alisema ukosefu wa walimu unasababisha watoto kushindwa kufanya vizuri katika mitihani yao hatimaye kujiunga na elimu ya sekondari bila maarifa ya kutosha.

"Watoto wengi wanafaulu kwenda sekondari ya Kigonigoni ingawa wengi wao hawana vitu vichwani mwao, hali inayosababisha kukatisha masomo yao kutokana na kutoelewa masomo vyema kulingana na misingi mibovu ya elimu ya msingi wanayopata," alisema Kajiru

Anastazia Msuya, mmoja wa wazazi hao, alisema kuna umuhimu wa serikali kuingila kati suala la walimu vijijini na kuwa na mpango maalumu wa kutoa elimu hasa kwa shule za msingi.

"Licha ya kuwa baadhi ya shule wameweka mpango wa kuajiri walimu waliopo kwenye mazingira yao, kuna umuhimu mkubwa wa serikali kuzitazama vyema vijijini ili kuleta tija. Hapa sasa ni jamii ya wakulima na wafugaji, mtoto anapofeli darasa la saba wanampeleka kulisha mifugo.

Hii ni hatari kwa taifa letu kwa baadaye," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Abdallah Mwaipaya, alisema tatizo la walimu ni kubwa hasa katika maeneo ya vijijini.

"Kuna shule unaweza kufika ukakuta walimu ni wawili, walimu ni watatu au wanne lakini niwapongeze wazazi kwa kushirikiana na kamati za shule huwa wanaajiri walimu waliohitimu ambao hawana ajira na hii inatusaidia kupunguza hayo makali.

"Lakini upungufu wa walimu hapa kwetu bado ni tatizo hasa maeneo ya pembezoni na hii pia inachangiwa na ongezeko la marekebisho ya miundombinu pamoja na kujengwa kwa shule mpya," alisema.

Mwaipaya alisema kwa sasa mahitaji ni walimu 1,027 lakini waliopo ni 650, hivyo upungufu ni walimu 377 ingawa bado serikali inaendelea kuajiri.

Pia alisema pamoja na matatizo hayo, bado Mwanga inafanya vizuri kwenye mitihani yote kuanzia shule za awali hadi kidato cha sita.

# Watu 400,000 kunufaika mradi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema kupitia mradi wa Tanzania Kidijitali wa ujenzi minara 758 ya mawasiliano nchini, unatarajia kuwanufaisha wananchi 421,259 wa mkoani Shinyanga baada ya minara 30 kujengwa mkoani hapa.

Alibainisha hayo jana alipofanya ziara mkoani Shinyanga akitokea mkoani Mwanza kukagua maendeleo ya ujenzi wa minara hiyo.

Waziri alisema serikali imepata Dolla milioni 150 za Kimarekani kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ili kuboresha mawasiliano hasa maeneo ya vijijini na kwamba Shinyanga inajengwa minara 30 katika kata 29 na vijiji 83.

"Utekelezaji wa mradi huu tunafanya kazi na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). Lengo ni kuhakikisha wananchi wa vijijini wanapata mawasiliano," alisema.

Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashimba, alisema katika miradi 30 ambayo inajengwa Shinyanga, tayari minara tisa imeshawashwa na kwamba kati ya minara 758 ambayo inajengwa nchi nzima, 186 imewashwa na inatoa huduma katika ujenzi wa minara hiyo wanashirikiana na kampuni za simu za mkononi.

Mkurugenzi wa Leseni na Ufuatiliaji wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), John Daffa, alisema hali ya mawasiliano kwa mkoa wa Shinyaga ni nzuri na kwamba kuna minara 257.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha,, aliishukuru serikali kwa kuimarisha mawasiliano hadi maeneo ya vijijini na kutoa wito kwa wananchi wawe na matumizi sahihi ya mitandao na kuahidi kusimamia kikamilifu ujenzi wa minara hiyo pamoja na kuimarisha ulinzi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanachama, viongozi msiturudishe tulipotoka

**WIKI** hii kumekuwa na matukio kadhaa kwenye upande wa soka hapa nchini ikiwa ni pamoja na usajili kwa klabu mbalimbali, lakini pia tumeshuhudia Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) likitoa ratiba ya michezo ya Ngao ya Jamii.

Matukio mengine ni kushuhudia klabu za Simba, Yanga na Azam FC zikienda nje ya nchi kwa ajili ya maandalizi kuelekea msimu mpya wa mashindano.

Matukio haya yote yana afya kwenye soka letu hasa katika kipindi hiki ambacho Ligi yetu inatajwa kuwa moja ya ligi bora Afrika ikishika nafasi ya tano.

Tunaona juhudi za dhati kutoka kwa wasimamizi wa soka letu, Shirikisho la soka Tanzania (TFF) na viongozi wa vilabu vyetu katika kulipeleka mbele soka letu ikichagizwa na juhudi za Serikali.

Kwa kipindi cha karibuni, Serikali imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha soka la Tanzania linazidi kupaa siku hadi siku huku likichagiza maendeleo ya vilabu vyetu kwenye nyanja ya kimataifa.

Hata hivyo, juhudi hizi zote zinataka kutiwa doa na masuala ambayo tulikuwa tukiyasikia na kuyaona miaka ya nyuma wakati soka letu bado halijawa kubwa kama sasa hivi.

Vitendo vya wanachama wa klabu kwenda mahakamani na kufungua kesi si ishara nzuri katika kukuza soka letu, linarudisha nyuma juhudi za wadau wote.

Tumesikia linaloendelea kwenye klabu ya Yanga baada ya baadhi ya wanachama wachache kwenda mahakamani kupinga uongozi uliopo sasa madarakani.

Inawezekana wakawa na hoja, lakini kupeleka mahakamani masuala ya michezo tena bila kupitia kwanza kwenye vyombo sahihi kwenye soka ni kutaka kulirudisha soka letu kwenye enzi za migogoro.

Nipashe tunaamini maendeleo ya sasa kwenye vilabu vyetu inatokana na utulivu kwenye uongozi na ushirikiano uliopo baina ya viongozi na wanachama.

Kuruhusu malumbano ya aina hii ni kuliandalia anguko soka letu, tufikirie kipindi cha nyuma hali ilivyokuwa wakati wa migogoro.

Kufanya vizuri kwa klabu zetu za Simba na Yanga kwenye mashindano ya Kimataifa kunatokana na utulivu uliopo sasa kwenye klabu hizo pamoja na uwekezaji mkubwa unaofanywa na wadhamini na wawekezaji.


Wanachama lazima watambue, sehemu zenye migogoro hakuna mwekezaji au mdhamini atakayethubutu kuweka pesa zake kuisaidia timu.

Furaha wanayoipata sasa hivi mashabiki kwenye klabu zao inatokana na uwekezaji unaofanywa na wadhamini wa wawekezaji, ndio maana leo hii tunaona timu za Tanzania zikicheza hatua ya robo fainali ya mashindano ya CAF, zamani haikuwa hivi.

Lakini pia mashabiki na wanachama wafahamu, ujio wa wadhamini na wawekezaji unatokana na amani na utulivu ndani ya klabu hizo, wanapaswa kudumisha amani na utulivu huo.

Tunaomba amani na utulivu kwenye klabu zetu ili bendera ya Tanzania iendelee kupeperushwa vyema kimataifa, kama kuna tofauti zozote, basi njia sahihi zifuatwe kutatua tofauti hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Hongera TFF, Bodi ya Ligi kukataa kupunguza wageni

**WAKATI** wa uzinduzi wa vifaa vya wasaidizi wa waamuzi vya njia ya picha za video maarufu kama 'VAR', hivi majuzi, pamoja na mambo mengine, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia, aliweka wazi kuwa wachezaji wa kigeni wataendelea kuwepo kwa idadi ile ile ya 12 na hata kanuni ya watakaotumika kucheza uwanjani itabaki vile vile kama zamani.

Karia akasema kuwa kuwepo kwa idadi hiyo ya wachezaji wa kigeni kumezifanya timu za Tanzania kufanya vyema kwenye mechi ya kimataifa za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, hivyo kupunguza idadi ni kujirudisha nyuma, kwani miaka ya nyuma klabu za hapa nchini zilipokuwa zikitegemea zaidi wachezaji wa ndani hata kutinga hatua ya makundi tu ilikuwa 'mtihani'.

"Kwa takwimu tulizonazo wachezaji wa kigeni hawajafika hata 70 kati ya wachezaji 600 ambao huwa wanashiriki Ligi Kuu kila msimu, hivyo wachezaji wetu wanatakiwa na wao watoke nje ili wakapate changamoto mpya na kuongeza uwezo wao na siyo sisi kupunguza idadi ya wachezaji wa kigeni," alisema Rais Karia na kuongeza,

"Tulipokuwa tukicheza na DR Congo na Zambia wachezaji wengi wa Tanzania walikuwa wa ligi ya ndani lakini walifanya vizuri sana kiasi cha kushangaza wengi, kwa sababu hawana tena ule woga wa kuogopa wachezaji wa kigeni, kila siku wanacheza na wachezaji hao hao ligi au wapo timu moja, hiyo imetusaidia sana kama taifa," alisema Karia.

Binafsi nampongeza sana Karia kwa kuliona hilo, na mara kwa mara wanaolitakia mema soka la Tanzania wamekuwa wakisisitiza kuendelea kuwapa nafasi wachezaji wa kigeni kuja nchini na kuendelea kulikuza soka la nchi na kuwakomaza wachezaji wetu.

Rais huyo alisema hayo kutokana na mapendelezo ya kanuni mpya ya Ligi Kuu msimu ujao, ambapo baadhi ya wadau walipendekeza kuwa wachezaji wa kigeni wapunguzwe kwa kile kinachodaiwa eti wanaziba nafasi za wachezaji wazawa.

Hii ni hoja mfu, kwa sababu kurudia alichosema Karia kuwa kuna wachezaji 70 tu kati ya 600, sasa ukifanya hesabu za kutoa hapo, bado wanabaki wachezaji wengi tu ambao wanaweza kuonyesha ubora wao na kuchaguliwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa.

Tatizo ni kwamba kuna baadhi ya watu wanadhani kuwa ili uchezee Stars ni lazima uwe Simba, Yanga au Azam, ambako huko ndiko kwa kiasi kikubwa wanasajili wachezaji 12 wa kigeni.

Klabu zingine zinasajili lakini hawafiki idadi hiyo, sasa wao wanadhani wale 12 wanazuia wazawa kupata namba na kuonekana. Lakini ukifanya uchunguzi mdogo tu, utagundua wachezaji wengi wa Stars wanatoka timu hizo hizo wanazoona zina wachezaji wengi wa kigeni yaani Simba, Yanga na Azam. Wale wale wachache tu wanaopata nafasi ndiyo tegemeo kwenye kikosi. Kwenye vikosi ambavyo wazawa wanajiachia, wapo kibao kwa idadi kubwa, bado hawapati nafasi ya kuchaguliwa timu ya taifa.

Ningekubaliana nao kama Simba, Yanga na Azam wasingekuwa na wachezaji Taifa Stars, halafu timu zingine ndizo zingetoa wachezaji wengi kwenye kikosi hicho, hapo tungesema wageni wanabana nafasi za wazawa.

Hii inaonyesha kuwa kiwango cha mchezaji binafsi ndiyo kinatakiwa.

Mimi nadhani hili limekuwa likipigiwa chapuo na baadhi ya mameneja wa wachezaji wa Kibongo ambao wanaona kama wachezaji wao hawapati nafasi ya kucheza ili kuwaongezea thamani, kwa sababu ya kuwepo kwa wageni wengi.

Mimi nawaasa tu mameneja au madalali wa wachezaji, wawafunde wachezaji wao kuongeza bidii ya mazoezi, kujitambua ndani na nje ya uwanja pamoja na wao wenyewe kuwatafutia timu nje ya nchi, badala ya kutaka kung'ang'ania waendelee kuwepo hapa hapa na kutaka wageni wapunguzwe.

# Wanahabari wanolewa elimu ya bima

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeipongeza Benki NMB kwa kukuza uelewa, ufahamu na elimu ya bima kwa jamii, huku ikivitaka vyombo vya habari nchini kuisaidia serikali kuibeba kwa uzito mkubwa ajenda hiyo ya kimkakati kuipeleka kwa Watanzania.

Pongezi na wito huo vilitolewa juzi na Naibu Kamishna wa TIRA, Khadija Said, alipokuwa anafungua mafunzo ya siku moja kuhusu huduma za bima mtawanyo (Bancassurance) kwa wahariri na waandishi waandamizi wa vyombo vya habari iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Khadija alimwakilisha Kamishna wa TIRA kufungua mafunzo hayo yaliyohusisha mada mbalimbali zikiwamo Dhana ya Bima, Benki Wakala wa Bima, Kazi za NMB Katika Uwakala, pamoja na Huduma za Kibenki na Bima Rafiki kwa Wanahabari zilizotolewa na Mkuu wa Idara ya Bima wa Benki ya NMB, Martine Massawe.

Akizungumza wakati wa ufunguzi huo, Khadija alisema NMB imechukua hatua kubwa kwa kutenga muda wa kutoa elimu kwa wahariri na wanahabari waandamizi ambao kwa kutumia vyombo vyao vya habari, wataongeza uelewa na elimu ya bima kwa jamii, ambalo ndio lengo la serikali.

“Niwapongeze NMB kwa mchango mkubwa katika kukuza uelewa wa elimu ya bima kwa jamii, inachofanya hapa ni kutekeleza Mpango Mkakati wa Serikali na Mpango Mkakati wa TIRA unaotaka kufikia mwaka 2030, asilimia 80 ya Watanzania wawe na elimu ya bima na asilimia 50 kati ya hao wawe wanatumia huduma za bima.

Alibainisha kwamba miongozo ya BenkiBima (BankAsurance) imetolewa kwa mujibu wa sheria, Kifungu cha 6(2) na Kifungu cha 11(A na B) vya Sheria ya Bima, Sura 314, ambacho kinataka mamlaka kuweka vigezo vya bima vinavyopaswa kuzingatiwa na taasisi za fedha katika utoaji bima.

Khadija alikiri kwamba BenkiBima ni sekta inayokua kwa kasi nchini, ikihusisha sekta ya fedha na sekta ya bima yenyewe, siri ya ustawi na ukuaji huo si tu ushirikiano baina ya taasisi hizo, bali pia mchango mkubwa wa vyombo vya habari katika kujenga na kuimarisha uelewa kwa jamii.

“Isaidieni serikali kutangaza umuhimu na soko la bima kwa Watanzania, kwani bima ni jambo la msingi na muhimu zaidi, inalinda mali zetu dhidi ya majanga, inalinda afya zetu dhidi ya maradhi, inasaidia kusomesha watoto hata wazazi au walezi wanapofariki dunia, zaidi inaongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla,” alisistiza.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema benki yake kama mdau wa maendeleo ya Watanzania, inatambua wajibu wake katika kuunga mkono juhudi za serikali kuendeleza sekta ya bima Tanzania, ambalo ni moja ya vipaumbele vya taasisi yao.

“NMB ni kinara wa elimu ya hima kwa wananchi, uthibitisho ni leseni namba moja iliyopewa na TIRA kufanya uwakala wa bima, huduma iliyozaa Huduma ya NMB UmeBima na tunaamini kupitia mtandao wetu mpana unaojumuisha matawi 231, tutasaidia kwa haraka kukuza uelewa wa masuala ya bima kwa jamii.

“Tunajua wajibu na jukumu letu, hatuwezi kuliacha jukumu la kuelimisha Watanzania juu ya bima kwa serikali pekee, na kwa kulitambua hilo, ndio maana sisi leo (juzi) tumeanza kuliongezea uelewa na ufahamu kundi la wanahabari, ili wao waizungumzie elimu ya bima kwa mapana kupitia vyombo vyao.

“Serikali inajua kupitia TIRA ilikuja na sheria ambayo iliwezesha benki pia kuuza bima, tukiangalia kitakwimu, idadi ya Watanzania wanaoutumia bima au wenye uelewa wa masuala ya bima ni ndogo, sisi tunayo fursa pana ya kuisambaza kwa jamii ili wawe watumiaji halisi wa huduma hizo,” alisema.

Aliongeza kwamba Sheria ya BankAsuarance ilitungwa mwaka 2019, lengo likiwa ni kuifaidisha sekta ya bima kupitia mtandao mpana wa matawi ya taasisi za fedha, huku akitolea mfano NMB, imesaidia kuipeleka elimu hiyo katika kila wilaya, hata katika maeneo ambayo huduma za bima hakuna.

“Kwahiyo, sheria hii ikaja kuwezesha kuisambaza huduma hii kwa jamii, kama tulivyosambaza matawi yetu na kweli imesaidia sana, kwani kwa sasa wananchi hawana tena haja ya kufika ziliko ofisi za bima, bali kwenye matawi yetu tu,” alibainisha Mponzi.

Alitolea mfano kwa kuyataja matukio ambayo jamii iliyokuwa na huduma za bima ilinufaika kupitia kampuni washirika wa bima kuwa ni moto ulioteketeza Soko la Kariakoo, Soko la Mlango Mmoja mkoani Mwanza, wakulima wa tumbaku Tabora, mafuriko ya Hanang’ na wafanyabiashara wa masoko mbalimbali yaliyoteketea kwa moto.



Mbunge wa Jimbo la Singida Magharibi, Elibariki Kingu (katikati juu ya meza), akizungumza katika mkutano wa hadhara wanakijiji cha Ihanja, wilayani Ikungi, akiwa katika ziara ya kuelezea utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye sekta ya elimu, maji, umeme na barabara jimboni humo, jana. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Kongani ya wazawa kuzalisha ajira 230,000

**Na Joseph Mwendapole**

KONGANI ya viwanda ya Modern Industrial Park ambayo inajengwa na Watanzania kwa gharama ya trilioni 3.5 inatarajiwa kutoa ajira 30,000 za moja kwa moja na ajira 200,000 za muda.

Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa Kongani hiyo, Tumaini Kabengula, alisema jana wakati wa ziara ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo, kwenye kongani hiyo iliyoko Mlandizi Mkoa wa Pwani.

Kabengula alimweleza Waziri Jafo kuwa kongani hiyo iko kilometa 71.5 kutoka katikati ya jiji la Dar es Salaam na kwamba matumizi mbalimbali ya eneo hilo la mradi ni pamoja na viwanda vikubwa, viwanda vya kati, viwanda maalum, maeneo ya kibiashara, miundombinu ya kijamii na matumizi ya ardhi ya umma.

Alisema gharama ya uwekezaji ni Dola za Marekani bilioni 1.4 sawa na Sh. trilioni 3.5 na ikikamilika itazalisha ajira za moja kwa moja 30,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 200,000 huku mapato ya mwaka yakitarajiwa kuwa dola bilioni 2.8 sawa na shilingi trilioni saba.

Alisema reli ya kisasa ya SGR kutoka Dar es Salaam hadi nchi za Afrika Mashariki inaungana na eneo hilo la viwanda kupitia kituo cha Ruvu na njia ya reli kutoka Ruvu itaungana na kongani hiyo kupitia bandari kavu watakayoijenga.

Naye Waziri Jafo alisema serikali itahakikisha umeme na maji vinafika kwenye kongani hiyo ili kuwezesha viwanda kuanza kazi.

“Nilitoa maagizo nikiwa Mkuranga kwamba mikoa itenge maeneo ya viwanda lakini Mkoa wa Pwani umeshapiga hatua kubwa sana kwa kuwa na maeneo mengi ya viwanda na mikoa mingine inapaswa kufanya hivi nawahakikishia na umeme na maji vitakuja mapema,” alisema.

Alisema mwekezaji huyo mzawa amechukua ekari 1,077 na amewekа miundombinu ya kuwawezesha wenye viwanda kwenda kuwekeza kwenye eneo hilo na kuweka huduma zote.

“Nimeangalia miundombinu mliyoweka maandalizi ni makubwa na nyinyi mnaonekana dhahiri mko makini na mnachofanya na uwekezaji mkubwa wa viwanda 222 vitakavyokuwa hapa si suala dogo nawapongeza.


“Mimi sitakubali mtu afanye utani na suala la viwanda nawahakikishia kwamba mko kwenye mikono salama kipaumbele changu cha kwanza ni kuwezesha viwanda na waambia wasaidizi wangu tuwe wawezeshaji na siyo wakwamishaji,” alisema.

Alisema viwanda 222 vitakavyojengwa kwenye eneo hilo vikianza kufanyakazi vijana watanzania watapata ajira kwasababu serikali haiwezi kuajiri vijana wote wanaohitimu vyuo vikuuu nchini.

“Nimesikia hoja ya maji, umeme viwanda haviwezi kufanyakazi bila kuwa na umeme na maji kwa hiyo mimi na wenzangu wizarani tutapambana kuhakikisha huduma hizo zinapatikana,” alisema.

## KABWELA

**Na Fadhili Mohammed**





Mwenyekiti wa Kamati ya kufuatilia wahitimu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Prof. Ambele Mtafya (wa pili kulia), akizungumza katika taasisi hiyo jana, wakati wa mjadala wa matokeo ya utafiti uliofanywa na taasisi hiyo kuhusu wahitimu wa chuo hicho kama wanaajirika au wanajiajiri. Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Taaluma, Dk. Petro Pesha. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali, wadau sarafu kidijitali wakutana kuweka mikakati

**Na Romana Mallya**

SERIKALI, taasisi za fedha, kampuni za simu pamoja na vyuo vikuu wamekutana kujadili teknolojia ya 'blockchain' na sarafu kidijitali zinazotumika duniani ili kupata uelewa wake na kuweka mikakati ya kuzitumia Tanzania kwa usalama na kwa faida zaidi.

Blockchain ni aina mojawapo ya teknolojia inayowezesha huduma mbalimbali kuwa za usalama zaidi na kupunguza mtu mmoja kuwa na taarifa peke yake.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Mhandisi Benedict Ndomba, aliyasema hayo jana katika warsha ya siku mbili, iliyondaliwa kwa kushirikiana na Chama cha Umoja wa Blockchain Afrika (UABA).

Mhandisi Ndomba alisema lengo la warsha hiyo ni kutoa uelewa na ujuzi wa pamoja kwa wadau wa sekta mbalimbali kuhusu matumizi ya teknolojia hizo mpya ili kila mmoja akatumie kulingana na mahitaji yake.

"Tutajikita katika mambo mawili, upande wa teknolojia blockchain na matumizi yake na upande wa 'digital currency' (sarafu kidigitali) ambayo ni sehemu mojawapo ya matumizi ya 'blockchain'.

"Tuna watu kutoka serikalini, benki, kampuni za simu na vyuo vikuu nia ni kujadili teknolojia hizi zinazoibukia ambazo ziko dunia nzima ili tupate uelewa wa pamoja na kuwa mkakati wa namna ya kuzitumia ndani ya nchi kwa usalama na kwa faida zaidi," alisema.

Kuhusu umuhimu wa teknolojia hiyo kwa sasa, Mhandisi Ndomba alisema ndiyo inayokua dunia nzima na watu wengi wanazitumia kutoa huduma mbalimbali, hivyo Tanzania haiwezi kukaa kimya ili watakapoitumia waifahamu.

"Ndiyo maana tumeita watu kutoka sekta mbalimbali tuchanganyike kujadili kwa pamoja kila mmoja kwa kazi anayofanya, waiangalie namna ya kuitumia ili kutoa huduma bora zaidi na kwa usalama zaidi kwa wananchi," alisema.

Kuhusu manufaa kwa Mtanzania wa kawaida, mkurugenzi huyo alisema kupitia teknolojia utoaji huduma itafanyika kwa urahisi na usalama zaidi kulinganisha na teknolojia za awali.

"Changamoto tuliyobaini ni uelewa na ujuzi juu ya teknolojia hii ndiyo maana tumeandaa warsha hii. Taasisi yetu eGA na taasisi zingine zinafanya utafiti kwenye teknolojia hii mpya, ili kuboresha utoaji huduma kwa wananchi na kwenda na dunia inakokwenda, kubaki nyuma maana yake fursa nyingi zinapotea," alisema.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Huduma za Teknolojia ya Janari na WMawasiliano (TEHAMA) katika mamlaka hiyo, Ricco Boma, alisema ni teknolojia hiyo inaruhusu watu wengi kuitumia badala ya mtu mmoja.

"Hii ni teknolojia ambayo ni salama kwa kila mtumiaji anaweza kutumia na taarifa zake kuwa salama bila mtu mwingine kuzifikia. Blockchain ni mtandao au mfumo ambao unaruhusu matumizi ya maombi mbalimbali na kuruhusu kila mtumiaji kuwa na taarifa zake," alisema.

Kuhusu sarafu kidigitali, Boma alisema kutokana na teknolojia inavyokwenda sasa, wanasema thamani ya fedha ni kuwa kidigitali.

"Unaipa thamani ya fedha kidigitali kulingana na fedha zilizopo. Unatumia sarafu kidigitali kama unavyotumia Dola ukiwa unafanya matumizi kidigitali, unatumia hizi sarafu za kidigitali ambazo zina thamani ya sarafu ambazo zipo kama Dola, Pound au Shilingi ya Kitanzania," alifafanua.

Alisema kupitia warsha hiyo, washiriki watapata fursa ya kuona namna hizo blockchain zinavyotengenezwa pamoja na kupata uzoefu wa sarafu kidigitali inavyofanya kazi na matumizi yake kwa kuangalia matumizi ndani ya serikali na taasisi binafsi na katika nyanja za uchumi.

Alisema mamlaka hiyo ina Kituo cha Utafiti na Ubunifu cha Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) hutafiti teknolojia hizo na kwa upande wa sarafu kidigitali wanashirikiana pia na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Boma alisema wametengeneza mifumo mbalimbali inayotumia teknolojia hizo ili kutumiwa na taasisi za umma.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ), Said Seif Said, alisema wanashirikana na eGA, hivyo kuna jitihada zilizofanyika ambapo watu kutoka Afrika Kusini wanawaelezea teknolojia hiyo.

"Jitihada hizi za uchumi kidigitali na mabadiliko ya TEHAMA lazima yafanyike kwa Tanzania nzima," alisema.

Mwenyekiti UABA, Yaliwe Milambo, alisema wamefurahi kufanya kazi na e-GA kutoa elimu namna teknolojia hizo inavyofanya kazi duniani, kuwezesha Bara la Afrika kuwa wadau katika mapinduzi ya kidigitali.

# Vyuo vyatoa ufadhili kwa asilimia 100

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Elimu ya Vyuo Vikuu nje ya Nchi, Global Education Link (GEL), imeanza kudahili wanafunzi papo hapo kwenye maonyesho yanayoendelea kwenye viwanja vya Maisara, Zanzibar.

Mkurugenzi Mtendaji wa GEL, Abdulimalick Mollel, alisema juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonyesho hayo yaliyoanza Julai 15 na yanatarajiwa kutamatika kesho.

Pia alizungumzia maonyesho yaliyoandaliwa na GEL yatakayofanyika Dar es Salaam Julai 23 na 24, mwaka huu na vyuo vikuu vingi vya nje kutoka India, China, Urusi, Iran, Uingereza, Canada na Australia vitashiriki.

Alisema kwenye maonyesho hayo kuna vyuo vya nje ya nchi ambavyo vimetoa udhamini wa asilimia 50 kwa wanafunzi wanaotaka kwenda kusoma kwenye vyuo hivyo na vingine vimetoa ufadhili wa asilimia 100.

"Tumeleta wawakilishi wa vyuo 20 kutoka Irani kuna ufadhili wa asilimia 100 analipiwa kila kitu na kuna vyuo ambavyo mwanafunzi atalipiwa asilimia 50 ya ada kwa hiyo mwanafunzi akija kwenye maonyesho haya akichagua kozi GEL tunamdahili hapahapa," alisema.

Alisema lingine la manufaa kwenye maonyesho hayo ni uhusiano wa vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi kwani uzoefu unaonyesha kuwa asilimia kubwa ya wahitimu wa vyuo vya nje ya nchi wanaajiriwa mara tu wanapomaliza vyuo.

"Mara nyingi wanafunzi wanaohitimu vyuo vya hapa nchini huanza kuhangaika kutafuta ajira kwenye maeneo mbalimbali na kulalamikia ugumu wa ajira wakati vyuo vya nje hali ni tofauti kwa wahitimu wao.

"Vyuo vya nje vinafanikiwa kutoa wahitimu ambao wanaajiriwa mara tu wanapohitimu ndiyo maana tumewakutanisha na vyuo vya ndani ili waweze kubadilishana maarifa, wao wanafanyaje kuwaandaa wanafunzi tunaangalia je ni suala la mitaala au ushirikiano mwema na taasisi za ajira," alisema.

"Kwa hiyo tulicholeta hapa ni ushirikiano baina ya vyuo hivi kama kuna chuo kikuu cha hapa ndani kilichoko tayari kushirikiana na chuo chochote cha nje watakutana na kubadilishana ujuzi na maarifa mbalimbali ili waweze kutoa wahitimu bora," aliongeza.

Alisema lingine ni fursa ya kupata udahili kwani baadhi yao wamekuwa wakikosa nafasi za kujiunga na vyuo vikuu kutokana na ufinyu wa nafasi kwenye baadhi ya kozi wanazoomba hasa zile za afya na uhandisi.

Mollel alisema idadi ya wanafunzi wanaoomba nafasi za kozi za afya na uhandisi ni wengi kuliko nafasi zilizopo hivyo kuna umuhimu wa kuwatafutia nafasi kwenye vyuo mbalimbali nje ya nchi.

"Tumekuja na vyuo hapa ambavyo vinaruhusu wanafunzi kudahiliwa hapa nchini akasoma kwenye chuo cha nje kwa miaka kadhaa kisha akarudi kumalizia elimu yake hapa Tanzania kwa hiyo sisi tunaona hii ni fursa kwa vijana wetu," alisema.

"Watanzania wachangamkie fursa za ufadhili wa vyuo vikuu wasidharau kwasababu tuna mtindo wa wa kudharau kwasababu ya kuogopa kujaza fomu zenye maelezo mengi lakini sisi tuna ofisi hapa Zanzibar waje tutawatafsiria maelezo hayo," alisisitiza.

Aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuonyesha utayari wa kushirikiana na Global Education Link kuendelea kuwatafutia fursa za elimu ya juu nje ya nchi.



# Polisi yachunguza utata kifo mtoto

**Renatha Msungu na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, limeanza uchunguzi wa utata wa kifo cha mtoto Telesphore Mwakalinga (4) aliyepotea Julai 17 na kukutwa amekufa usiku wa kuamkia jana katika eneo la nyumba 300 Kisasa jijini hapa akiwa amekwata mkono na kuondolewa sehemu zake za siri.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Theopista Mallya, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu kuhusu tukio hilo juzi, alisema jeshi limepokea taarifa ya kifo cha mtoto huyo na sasa linaendelea na uchunguzi kubaini chanzo cha mauaji hayo.

"Kweli tukio hilo limetokea katika eneo la nyumba 300 ambapo mtoto huyo na familia yake walikuwa wanaishi lakini alipotea Julai 17 na usiku wa kuamakia leo (jana) alikutwa amekufa," alisema

Kamanda huyo alisema Jeshi la Polisi likiwa katika doria kwenye eneo hilo, mmoja wa askari alimwona mbwa akiwa na kitu mdomoni ndipo walipomsogelea na kubaini kuwa ni mwili wa mtoto mdogo akiwa amefariki dunia.

Alisema mwili huo huyo ulikutwa ukiwa umekatwa mkono pamoja na sehemu za siri zikiwa zimenyofolewa ndipo taarifa hiyo iliwasilishwa ofisini kwake.

Kamanda Mallya alisema mtoto huyo alipotea juzi majira ya saa 12 jioni na mwili wake ulipatikana saa nne usiku akiwa amefariki pamoja na kutolewa baadhi ya viungo vyake.

Kamanda Mallya alisema bado kuna utata wa kifo cha mtoto huyo asiye na hatia yoyote kilichosababishwa na watu wenye maslahi yao binafsi. "Jeshi la polisi kutokana na tukio hili la utata tunaendelea kufanya uchunguzi ili kubani nini sababu ya kifo chake kutoka kwa madaktari ili hatua nyingine zichukuliwe na wote waliohusika wakamatwe,"alisema

Aidha, alisema wazazi wanapaswa kuwaangalia watoto wao ifikapo majira ya usiku ikiwemo kutoa taarifa Jeshi la Polisi pale wanapoona kuna watu wanazunguka pasipo na kazi yoyote kwenye mitaa mbalimbali.

Kamanda Mallya alisema mwili wa mtoto huyo umehifadhiwa katika chumba cha kuhifadhia maiti katika hospitali ya rufaani ya mkoa wa Dodoma, huku Jeshi hilo likisubiri taarifa kutoka kwa daktari ya chanzo cha kifo cha mtoto huyo.

# CHADEMA yalia viongozi kukamatwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Singida kimelalamikia hujuma za kukamatwa ovyo kwa viongozi wanaoendesha usajili wa wanachama kidijitali unaoendelea kwenye majimbo saba ya mkoa huu.

Kutokana na hali hiyo, CHADEMA imeliomba Jeshi la Polisi Mkoa wa Singida kuingilia kati chokochoko hizo ili kuepusha uvunjivu wa amani unaoweza kutokea mkoani hapa.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Jackson Jingu, akizungumza juzi na waandishi wa Habari, alisema chama hicho kina usajili wa kufanya siasa kama vyama vingine kwa uhuru na haki hivyo hujuma wanazofanyiwa katika zoezi la usajili wanachama halina afya kisiasa.

"Tunatoa taarifa kwa Jeshi la Polisi na tunapotoa taarifa hizi wawe wanasimamia misingi na utawala bora kwa kuwasihi wenzetu wa chama tawala wasifanye mambo haya ambayo yanaleta taharuki na tunamwomba RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa) achukue hatua," alisema.

Jingu alisema CHADEMA katika Mkoa wa Singida haipendi kuona kunatokea vurugu kwa sababu ya hujuma wanazofanyiwa badala yake kila chama kiachwe kifanye siasa kwa kuzingatia misingi ya katiba na sheria kunadi sera zake na kitakachokubaliwa wananchi watakipa ridhaa ya kuongoza nchi.

"Hatutakubali kuona waandikishaji wetu wa wanachama kidijitali ambao wametoka makao makuu wanaendelea kusumbuliwa na kufuatwa na pikipiki za chama tawala ili kuwakatisha tamaa wasifanikishe zoezi hili," alisema Jingu.

**KAULI YA NAPE**

Kuhusu kauli iliyotolewa na Waziri wa Habari,Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye ya ushindi nje ya boksi la kura, Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Singida alisema kauli yake haiwatishi na badala yake imewasaidia kujua ukweli na hivyo kujipanga katika chaguzi zijazo.

Naye Katibu wa CHADEMA Jimbo la Singida Mjini, Hamis Nkua, alisema mbali na changamoto ya waandikishaji kupata usumbufu lakini pia bendera za chama hicho zilizopo mitaani zimekuwa zikishushwa jambo ambalo si zuri.

Nkua alisema wanaofanya vitendo hivyo lazima watambue kuwa kila chama kina haki ya kuweka bendera zake kwenye mitaa na maeneo mbalimbali ikiwa ni hatua mojawapo ya kujitangaza kwa wananchi.

Naye mtia nia ubunge katika jimbo la Iramba Magharibi, Joseph Salum, alisema amefanya ziara katika kata kadhaa za jimbo hilo na kujionea jinsi waandikishaji wanachama kidijitali wanavyopata usumbufu wa kukamatwa na kuwekwa ndani

Salum alisema wanaofanya hujuma hizo watambue kwamba Chadema ni chama ambacho kimeandikishwa kisheria hivyo kina haki ya kufanya siasa katika katika nchi hii.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Eliakim Maswi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kufunguliwa kwa jukwaa la ununuzi wa umma la Afrika Mashariki litakalofanyika mkoani Arusha Septemba 9 hadi 12 mwaka huu. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Teknolojia mpya ujenzi yaonyesha matumaini

**Na Renatha Msungu,** CHAMWINO

TEKNOLOJIA ya kisasa ya ujenzi wa barabara kwa kuboresha udongo kabla ya kuweka lami juu ijulikanayo kama 'Ecoroads' imeonyesha matumaini katika miezi sita ya majaribio.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia miundombinu, Mhandisi Rogatus Mativila, alisema hayo jana baada ya kutembelea barabara zilizojengwa na teknolojia hiyo yenye urefu wa kilometa 6.95 wilayani Chamwino.

Mhandisi Mativila alisema lengo kubwa la kutembelea barabara hizo ni kujionea mafanikio ya matumizi ya teknolojia hiyo ambayo pia inajaribiwa katika wilaya mbalimbali nchini na inatekelezwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

"Lengo la kuja kutembelea barabara hii hapa Chamwino ni kuangalia mafanikio ya matumizi ya teknolojia hii ya kisasa ya kuboresha udongo kabla hatujaweka lami juu inayotekelezwa na TARURA," alisema.

Alisema teknolojia hiyo pia inafanyiwa majaribio Mufindi, Rufiji na maeneo mengine ili kuitumia sehemu zingine na imepunguza gharama na muda wa ujenzi wa barabara.

"Barabara hii iliyojengwa inaonekana ni imara na pia sehemu nyingine ya kilometa 1.3 haijawekwa lami ila udongo uliokuwa pale umechanganywa na kemikali ambayo tunaendelea kufanyia majaribio tuweze kuona mafanikio yake.

"Tunafanya hivyo ili kuona kabla haujafunika na tabaka la juu inayozuia maji na vitu vingine je! inaweza kudumu kwa muda mrefu na tayari imeshakaa kwa muda wa miezi sita na tumekuta bado ipo imara kwahiyo inatuonesha hii kemikali inayotumika inahimili na malighafi ni nzuri lakini bado tunaendelea kuiangalia ili tukiona imefanikiwa itatumika kwa kiwango kikubwa kwenye ujenzi wa barabara zinazosimamiwa na TARURA," alisema.

Wakati huo huo , Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, alisema teknolojia hiyo wilayani Chamwino ni sehemu ya majaribio na tayari wameshafanya katika maeneo mbalimbali ikiwamo barabara ya Ilazo -Dodoma (Km moja) Sawaka - Mkonge- Iyegeya- Lulanda - Mufindi (km. 10.4) na Utete - Kingupila - Rufiji (km. 32).

"Tangu ujenzi kukamilika hapa Chamwino tayari imeshapita zaidi ya miezi sita lakini bado barabara zina hali nzuri hivyo sasa hivi tunaendelea na tathimini ya mafanikio ya hii teknolojia yenyewe ili hapo baadae tuje tuishauri serikali kama teknolojia hiyo iendelee kutumika katika ujenzi na matengenezo ya barabara zetu," alisema.

Alifafanua kuwa lengo la kuwa na hizo teknolojia ni kupunguza gharama, kuwa na muda mfupi wakati wa ujenzi pamoja na utunzaji wa mazingira.

Mhandisi Seff aliongeza kuwa licha ya gharama kuwa ndogo, bado kuna tofauti kulinganisha na ujenzi wa kawaida na faida ya teknolojia hiyo inaonekana moja kwa moja katika muda wa utekelezaji kuwa mfupi akitolea mfano barabara hiyo ya Chamwino ambayo mkataba wake ulikuwa wa mwaka mmoja ila wameweza kujenga na kukamilisha ndani ya miezi sita.

Fundi wa magari kutoka mtaa wa Mshikamano, Songo Yusufu, alisema barabara hizo za sasa ni bora kuliko za mwanzo ambapo ujenzi wa barabara hizo zimerahisisha kufikiwa na wateja wake kwa urahisi kwani awali barabara ilikuwa na vumbi pamoja na mashimo mengi.





# Mbunge ataka ubunifu miradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Mjini Magharibi, Tauhida Galos Nyimbo, amewataka wajasiriamali kubuni mbinu mbadala za kuwaletea maendeleo katika familia zao.

Aliyasema hayo Mazizini nje ya mji wa Zanzibar baada ya kukabidhi majiko ya gesi na sare kwa wajasiriamali wa jiko la wavuvi Mazizini Wilaya ya Magharibi B, Unguja.

Nyimbo alisema serikali zote mbili zimeweka mikakati ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, hivyo ni vyema kujiunga na kuanzisha miradi ya maendeleo ikiwamo ya ujasiriamali.

Pia aliwataka kujali na kuthamini kazi ili kufikia malengo waliyojipangia ya kujikwamua na umasikini, tatizo linaloiathiri jamii hususan wanawake.

Mbunge huyo aliahidi kuzifikisha sehemu husika changamoto zinazowakabili wajasiriamali hao ili ziweze kutafutiwa ufumbuzi wa haraka.

Mkuu wa Jiko la Mazizini, Hashim Omar Haji, alisema umoja huo umewaunganisha wanawake kisiasa, kiuchumi na kimaendeleo.

Aliwataka kuendelea kushirikiana ili kuzidi kukuza umoja na kupata mahitaji muhimu ikiwemo kusomesha watoto wao.

Wajasiriamali wa eneo hilo walitaka kupatiwa ufumbuzi matatizo yanayowakabili ikiwemo vitendea kazi, ukosefu wa wafadhili na mafunzo ya ujasiriamali ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Tatu Ali, mmoja wa wajasiriamali hao, akizungumza kwa niaba ya wezake, alisema majiko hayo yamekuja muda muafaka ambayo yatawasadia katika shughuli zao za mama ntilie na kuachana na matumizi ya kuni kwa kupikia.

Alimpongeza mbunge huyo kwa kufanya ziara hiyo na kumuomba kuwaunga mkono kwani kikundi hicho kimekuwa mkombozi mkubwa wa kujipatia kipato na kuepukana na utegemezi.

# DMI yasema hakuna kizuizi kozi ya bahari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk. Willfred Kileo, amesema hakuna vizuizi kwa wasichana na wanawake kujiendeleza katika elimu ya juu katika fani ya ubaharia na mambo ya bahari.

Amesema serikali nyingi duniani na mashirika ya kimataifa ya mambo ya bahari yanaweka msisitizo kwenye kutunza haki na shughuli zingine zinazowahusu.

Dk. Kileo aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari pamoja na wananchi waliotembelea banda la DMI katika maonesho ya taasisi za elimu ya juu yanayofanyika Maisara, mjini Unguja.

Alisema ubaharia na mambo ya bahari ni kazi kama zingine, hivyo ni vyema wanawake kuitumia fursa ya uchumi wa buluu na kujiunga na chuo hicho kupata elimu ya bahari kwa ajili ya kupata mafanikio.

Dk. Kileo alisema bado mwitikio ni mdogo katika fani ya ubaharia hasa kwa wanawake, hivyo ni vyema kuwatia moyo kujikita katika masomo ya sayansi ili kufikia viwango vya ufaulu na kujiunga na fani hiyo.

Aidha, alisema kuna dhana potofu kwa baadhi ya wazazi ya kutokuwa na ujasiri wa kuwaruhusu watoto kujiunga na fani ya ubaharia kutokana na mfumo dume uliojengeka katika jamii. Alisema DMI chuo pekee kinachozalisha wataalamu wa bahari ambao wamekuwa wakifanya vizuri katika maeneo mbalimbali na kusaidia taifa katika kukuza uchumi.

Chuo hicho, alisema kilianzishwa mwaka 1978 kikiwa na wataalamu 12 na sasa mafanikio makubwa yamefikiwa hadi kuzalisha wataalamu 5,177.

Dk. Kileo alisema chuo hicho huzalisha mabaharia wenye uwezo ambao wanafanya kazi katika meli kubwa zinazosafirisha bidhaa na wafanyakazi wanaotoa huduma katika meli za abiria zilizoko nchini.

Hata hivyo, alisema hivi sasa chuo kinatoa mikopo ya elimu ya juu ya aina mbalimbali kwa wanafunzi ili kusoma na kuchukua kozi zitakazowawezesha kufanya kazi na kupata ajira.




Meneja wa taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation, Sandra Oswald (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, wakati wa uzinduzi wa ziara ya 'Building Brains Tour' kwa ushirikiano na shirika la kuhudumia watato kielimu la Ubongo itakayofanyika katika mikoa ya Mara na Arusha. Wengine ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma (katikati) na Mkuu wa Kitengo cha Usanifu wa Ubongo, Micheal Baruti. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Othman asema rushwa bado kikwazo Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema tatizo la rushwa bado ni changamoto kubwa licha ya serikali kuendelea na juhudi za kuweka mikakati na mbinu bora kadhaa za kupambana na suala hilo.

Othman aliyasema hayo jana alipokutana na Balozi wa Switzerland Tanzania, Didier Chassot, aliyefika ofisi kwake, Migombani, mjini Unguja kumuaga baada ya kumaliza muda wake wa miaka minne ya ubalozi nchini.

Alisema serikali imewaka sheria na taratibu madhubuti za kupambana na suala hilo sambamba na kuijengea uwezo mamlaka inayohusika na kupambana na tatizo hilo ili kuhakisha uwajibikaji bora ili kuidhibiti rushwa Zanzibar.

Othman alisema suala la rushwa Zanzibar ni eneo linalohitaji jitihada za wadau na washirika ikiwamo misaada ya kifedha katika kuweka nguvu na mikakati imara zaidi ya uwajibikaji wa pamoja katika kupambana nayo.

Kuhusu kuimarisha demokrasia na uchaguzi mkuu wa mwaka ujao, Othman alimweleza Bolozi Chassot kwamba kuna matumaini ya uchaguzi kuwa bora kuliko uchaguzi wa uliopita kwa kuzingatia kwamba mabadiliko hayawezi kutokea kwa siku moja.

Hata hivyo, alisema ni muhimu kujengwa uelewa kwa wananchi na viongozi sambamba na kuwapo majadiliano ya umma juu ya haja, umuhimu na namna bora ya kuimarisha masuala ya uchaguzi wa kidemokrasia nchini.

Kuhusu uwajibikaji wa viongozi na wananchi, alisema kwamba hilo ni jambo muhimu katika kuhakikisha kasi ya maendeleo ya nchi na hakuna taifa lolote duniani linaloweza kupiga hatua ya kimaendeleo bila kuwepo uwajibikaji na kujengwa taasisi imara za utoaji wa huduma kwa wananchi.

Akizungunzia mabadiliko ya tabianchi, Othman alisema maeneo karibu 148 katika mashariki ya visiwa vya Unguja na Pemba yameathiriwa na tatizo hilo yakiwamo mashamba ya chumvi Pemba na zaidi ya wananchi 2,000 wanaojishughulisha na kazi hiyo, maeneo yao yameathiriwa.

Naye Balozi Chassot aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na ushirikiano wake kwenye maeneo mbali mbali ikiwemo afya, utawala bora na masuala ya kupambana na rushwa nchini.

Aidha alisema serikali ya nchi yake inatambua changamoto ya mabadiliko ya tabianchi na kwamba suala hilo ni miongoni mwa vipaumbele muhimu vya nchi yake katika kushirikiana na nchi mbali mbali ikiwemo Zanzibar na Tanzania kwa jumla katika kupambana nalo.



SIMI PUNGUZA MANENO UK.14

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI JULAI 20, 2024

# Kuna la kujifunza



MAJUZI mastaa wa muziki wa Bongo fleva, Billnas na Nandy, wametimiza miaka miwili tangu wafunge ndoa ambayo sherehe zake zilizua gumzo.

Pamoja na sherehe ya harusi yao kuvunja rekodi, lakini watu walivutiwa na kile kilichoendelea katika maisha yao ya ndoa.

Hata hivyo, wanandoa hao katika kipindi hicho wametoa funzo kwa mastaa wenzao kwamba ndoa si lele mama, inahitajika subira, uvumilivu na kuheshimiana.

Wanatakiwa kujifunza kuwa maisha ya kuchukuana na kuachana kama nguo za mitumba, hayawezi kudumisha ndoa. Nandy na Billnas kwao imekuwa tofauti, kwani licha ya kuwa na mtoto mmoja, kila siku wanajitengeneza upya na kugeuza kurasa zao za kijamii kama uwanja mpana wa upendo.

Ni jambo la kawaida kuona wawili hao wakichapisha jumbe za kimahaba kwenye mitandao, huku kila mmoja akimshukuru mwenzake kwa kumvumilia kutokana na madhaifu yake. Billnas na Nandy wamekuwa walimu wazuri wa kuyageuza mabaya na kuwa mazuri, kiasi ambacho ndani ya miaka hiyo hakuna hata mmoja aliyejuna na kuanika mabaya ya mwenzake. Kila mmoja alishukuru kwa kile anachofanyiwa.

Hayo machache ambayo wameyaonyesha, mastaa wengine wameshindwa kuyamudu na kusababisha ndoa zao zimesambaratina na zile zilizobaki zikining'inia kwenye kamba dhaifu na wakati wowote zitaanguka.

BASI SAWA

## Man Fongo hana kosa kwa hili...




STAA wa Muziki wa Singeli, Man Fongo, amesema hajali watu wanavyoujadili wimbo wake mpya ambao umejaa utata.

Akizungumza hivi karibuni, Man Fongo, amesema wimbo huo hauna tatizo kwa sababu amezungumza vitu vya kawaida katika jamii na kutaja kwake baadhi ya wasanii kwake sio jambo geni.

"Watu wanazungumza mengi kuhusu wimbo wangu, lakini nashukuru mashabiki wengi wameupokea kwa furaha na unafanya vizuri katika majukwaa ya muziki," amesema Man Fongo.

## ZIFF yawatangaza waigizaji kimataifa

WASANII wa filamu wa Tanzania, wamepongezwa kutokana na kulitumia vyema Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar (ZIFF), kujitangaza ulimwenguni.



Akizungumza hivi karibuni, Ofisa Mtendaji wa ZIFF, Joseph Mwale, amesema kwamba tangu kuanzishwa kwa tamasha hilo, idadi ya filamu kutoka ndani ya nchi zimeongezeka na kuziwezesha kupata tuzo mbalimbali.

Mwaka huu, jumla ya filamu 70 kutoka mataifa mbalimbali duniani zimeteuliwa kushiriki tamasha hilo litakalofunguliwa Agosti Mosi mwaka huu.

"Nataka niwapongeze wasanii, waongozaji na wadau wa filamu nchini kwa kutumia vizuri uwepo wa tamasha hili hasa kwa kuongeza ubora na hatimaye kupata tuzo ambazo huko nyuma ilikuwa vigumu," amesema Mwale.

Mwaka huu vipengele vitakavyoshindaniwa ni, filamu bora ndefu, fupi bora, filamu bora ya Afrika Mashariki na Mwigizaji bora wa kike na kiume Afrika Mashariki.

Pia, Mwingizaji bora wa kike na kiume Tanzania, tuzo ya Mwenyekiti, mafanikio katika maisha ya filamu na chaguo la watu ambayo itatokana na tamthilia zinazorushwa katika televisheni katika nchi za Afrika Mashariki.



# Tanasha aumia kuwa mbali na Diamond

MWANAMUZIKI kutoka Kenya, Tanasha Donna, amesema jambo linalomuumiza katika maisha yake ni kumpa malezi mtoto wake mbali na baba yake mzazi.

Akizungumza hivi karibuni, Tanasha amesema kwamba licha ya mzazi mwenzake Diamond Platnumz, kusaidia malezi kila mara ukweli unabaki kwamba wazazi wote wakiishi pamoja ni kitu cha kujivunia.

"Wakati ndio mara yako ya kwanza kuwa mama, unatoka katika ndoa yako, nikimaanisha kwamba ndio mara ya kwanza pia kuwa 'single mother', ila ninapozungumzia kuhusu hilo muda mwingi ni mimi ninaishi naye hata kama anamtembelea babake mara kwa mara, lakini nafikiri changamoto ni kubwa," amesema.



# Binamu kinyama cha hamu

Na Adam Fungamwango

PENZI halichezewi na wala halijaribiwi. Ndivyo unavyoweza kusema. Ni msemo wa wahenga tangu enzi na enzi.

'Binamu' ni filamu iliyochezwa na wasanii Affan Jamal, Diana James, Ahur James, Jumanne Simba na wengine. Ni filamu inayotoa funzo watu kuwa waangalifu sana wanapokuwa kwenye mahusiano au ndoa.

Usimfanyie kitu mpenzi wako ambacho wewe hutaki kufanyiwa. Kwa sababu ipo siku utakuja kufanyiwa wewe ukakasirika.

Jamaa mmoja anaitwa Sharukhan. Huyu ana mkewe Zaina. Kwa sababu wamekaa muda mrefu bila ya kuwa na mtoto, Sharukhan anamwambia mkewe ameleta dada yake binamu ili angalau nyumba ichangamke.

Analetwa dada mmoja anaitwa Ashura. Ni Ashura, Ashura kweli. Kipande cha dada, kimeumbika.

Siku si nyingi, mke wa Sharukhan akaanza mambo yanabadilika. Mara kwa mara akawa wanawakuta wanadekezana, wamekumbatiana. Zaina anapoulizwa akaambiwa kuwa hiyo ndiyo tabia yao tangu utotoni kwa sababu wamekuwa pamoja.

Hali hiyo ilimfanya Zaina asipate usingizi. Akawaza na kuwaza. na yeye akakata shauri ya kumpigia kaka yake binamu aje. Sharukhan akafungwa kamba kuwa kaka wa mkewe, yaani shemeji yake anakuja kusalimia. Lengo ilikuwa ni kulipiza kisasi.

Kaka akafika. Kinachotokea ni kama kile ambacho Sharukhan na Ashura wanafanya. Majirani wanaona kila kitu. Zaina na kaka yake wanacheza ngoma, kuimba na kukumbatiana hadharani. Sharukhan anaambiwa yote.

Mapenzi yanauma. Hali ya jamaa ilianza kubadilika. Sasa hata dada yake binamu, akitaka kudekezana, Sharukhan hataki. Akili yote ni kwa mkewe akiona kabisa sasa anaibiwa.

Akaitisha kikao. Akaanza kutoa kilicho moyoni mwake. Mkewe akasema amefanya vile kwa sababu ya kulipa kisasi cha kile ambacho anafanyiwa ndani ya nyumba hiyo.

Alivyoona haelewi, mwenendo wa mumewe na dada yake binamu, basi akaona na yeye akamlete kaka yake binamu kwa ajili ya kuigiza kama wanavyofanya mumewe na Ashura ili kuweka mambo sawa. Akamwambia mumewe kuwa hata yeye alikuwa anaumia sana kwa alivyokuwa anafanyiwa.

Mwisho wa siku, kaka binamu wa Zaina ilibidi arudishwe kwao, Ashura akatafutiwa mchumba ambaye ni rafiki wa Sharukhan, yeye mwenyewe akabaki na mkewe.





# Jay Melody anawakaribisha

MKALI katika muziki wa Bongo Fleva, Jay Melody, ametamba kutoa burudani ya aina yake leo katika uzinduzi wa albamu yake mpya Therapy utakaofanyika katika ukumbi wa Ware House jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, amemshukuru msanii mwenzake Diamond Platnumz, kwa kumuunga mkono katika onyesho lake na kuwaomba wasanii wengine kujitokeza kwenda kukesha naye.

"Nimepata baraka ya kaka yangu Diamond Platnumz, namshukuru sana na nawaomba wasanii wengine kuja kuniunga mkono katika onyesho langu," amendika Jay Melody kwenye ukurasa wake wa Instagram.

# Dunia rangi rangile

Na Adam Fungamwango

UKISIKILIZA hadithi nyingi na mambo mengi ya zamani na hata ukisoma kwenye vitabu mbalimbali vyenye kuheshimika, utagundua hakuna kitu kipya hapa duniani kinachofanyika.

Yote ni yale yale tu. Ni kama vile wanasayansi wanavyosema dunia inajizungusha yenyewe kwenye mhimili wake na kweli yote yanayofanyika yanajirudia tu.

Tena kuna vitu vingine vilifanyika zamani hadi leo hii havijafanyika tena. Vinavyoendelea kujirudia ni baadhi ya mambo machache tu yaliyofanyika miaka milioni nyingi huko nyuma.

Mmoja akaandika shairi hili. Dunia rangi rangile, methali hii muhimu, usione jambo lile, ukadhani la dawamu, kila chombo na wimbile, hilo mwenzangu fahamu.

Usione mtu yule, hana maisha matamu, ukamsonda kwa ndole, kama kaila haramu,Aso hili ana lile, nakujuza muadhamu. Leo tutaziangalia nyimbo zinazozungumzia dunia, raha, matatizo yake na vituko zilizotungwa miaka ya 1980 mwanzoni hadi mwishoni.

**Dunia Duara-Dede**

Shaaban Dede akiwa na Bima Lee, alitunga kibao cha 'Dunia Duara'. Hiki kinazungumzia juu ya mtu anayechekwa na wenzake kuwa hana kitu.

Lakini mwenyewe anajipa matumaini kuwa dunia ni duara na huzunguka, hivyo anajua kesho atapata kwa jinsi anavyojituma. Anasema jua halina mpaka, huangaza pote, ipo siku na yeye ataangaziwa, kwani kama samaki baharini, wadudu mapangoni na wanyama porini wanaishi, basi kwa kudra za Mungu, yeye atakosa vipi?

**Dunia Uwanja wa Fujo-Marijani**

Jabali la Muziki Marijani Rajab, yeye akatunga kibao cha 'Dunia Uwanja wa Fujo'. Anawatahadharisha wote wanaojimwambafai na kuiona dunia kama yao, kuwa walikuwepo watema, wafalme wenye nguvu, lakini leo hii hawapo.

Alikuwepo Firauni, Hitler, Nduli Idd Amini ambao historia ni inasema ni moja kati ya viongozi wababe kuwahi kutokea duniani, lakini kwenye dunia hii hakuna mbabe kushinda Mwenyezi Mungu. Wote wamekufa Kwa maana hiyo, watu wanaopewa dhamana ya kuongoza popote pale, kuishi vizuri na watu, kwa sababu ubabe hauna una mwisho kwenye hii dunia, 'kula ugali wako ukalale'.

**Dunia-Remmy Ongalla**

Remmy Ongalla kwenye fasihi yake ya wimbo huu wa 'Dunia' anasema yote ambayo binadamu atakayofanya hapa duniani, ikiwa ubaya au wema, atalipwa hapa hapa ulimwenguni.


Anasema kwa Mungu hatupajui, hivyo binadamu anatakiwa kutenda wema, kwani kuna baadhi ya watu hudhulumu wengine kwa vyeo vyao, wadhifa, pesa na umaarufu.

**Dunia-TX Moshi William**

Akiwa na bendi ya Polisi Jazz, kabla ya kujiunga bendi ya Juwata Jazz, alitunga kibao kisemacho 'Dunia'. Anauliza, mwezi na nyota usiku zinang'aa bili yake analipa nani? Na ilitakiwa kabisa aulizwe anayelipwa bili ni nani? Huyo ni mwenyezi Mungu. Yeye kila kitu hutoa bure kwa waja wake.

**Dunia Imani Imekwisha-Marijani**

Hapa Marijani amerudi tena hapa na wimbo wa 'Dunia Imeni Imekwisha'. Yoyote aliyedhani eti sasa ndiyo kuna dhana hiyo, lakini hata miaka ya 1970 hadi 1980, kulikuwa na matendo kiasi cha kuonekana dunia imani yake ni ndogo. Watu wanaibiana. Wanatapeliana. Wanadhulimiana. Kuna wanaodhulumu watoto yatima. Wanaotaka kuwaua wazazi wao ili warithi mali na mengine mengi.



SHABAN DEDE




# Simi punguza maneno

MWIMBAJI wa Nigeria, Simi, amejitokeza kwenye mitandao ya kijamii, akielezea kusikitishwa kwake kutokana na watu kumchukulia tofauti kuhusu kauli yake kwamba hasikilizi muziki.

Mwimbaji huyo alikosoa vyombo vya habari kwa kutangaza tofauti na alichosema na kuibua hisia mbaya kwa watu.

"Nachukia kufanya mahojiano haya ya kijinga wakati mwingine kwa sababu hawakujali na kukuunga mkono. Watasema uwongo au watachapisha vitu nje ya muktadha ili watu warundikane na kukugombeza," ameandika Simi.



## Joe Jonas atumia albamu kujiliwaza

MWANAMUZIKI wa Marekani, Joe Jonas amesema albamu yake mpya ilitumika kama matibabu ya msongo wa mawazo baada ya kuachana na mpenzi wake Sophie Turner.

Amesema kwa miaka mitatu alikuwa akipambana na tatizo hilo, lakini kutokana na kazi aliyoifanya ndani ya albamu hiyo imemfanya kufarijika.

Joe ameeleza kwamba jambo hilo awali aliliona kama la kibinafsi na alihisi anapitia kipindi kigumu akipitia tangu yeye na mkewe walipotengana.

## Rema kumbe unamjua Mungu

NYOTA wa Afrobeat, Rema amefunguka kuhusu anavyokabiliana na shinikizo na ukosoaji unaotokana na umaarufu wake.

Rema amefichua kuwa kila wakati anafanya maombi na kupata ushauri kutoka kwa marafiki zake pale anapopambana na hali hiyo.

"Kwanza ningesema kwamba naomba sana, namwomba Mungu na namuomba hekima, mwongozo, maarifa na uvumilivu, na ninawashukuru watu ambao ninao karibu kunisaidia," amesema Rema.





## Kate hataki visingizio

MWIGIZAJI mkongwe wa Nigeria, Kate Henshaw, amekasirishwa na baadhi ya watu wanaoweka dhana kwamba kuchelewa ni jambo la kawaida kwa Waafrika.

Katika chapisho lake kwenye mtandao wa X, amesema dhana hiyo mara nyingi huwa ni kisingizio kwa ajili ya kuhalalisha kuchelewa katika jamii za Kiafrika.


"Hakuna kitu kama katika jamii ya Afrika. Ukichelewa huwa kama kitendo cha kukosa adabu na heshima, hivyo haina nafasi kabisa," amewaambia wafuasi wake.

## Ini anapambana na uvimbe

MIAKA mitatu baada ya kufanyiwa upasuaji wa kuondoa uvimbe tumboni, mwigizaji wa Nigeria Ini Dima-Okojie, ametangaza kuwa tatizo hilo limerudi tena.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, msanii huyo aliwahutubia wafuasi na mashabiki wake kuhusu changamoto anazokabiliana nazo na mipango yake kusonga mbele kimaisha, alifafanua.

"Nataka niwaambie kitu, kwamba kabla ya mwisho wa 2020, nilifanywa upasuaji wa kuondoa uvimbe. Upasuaji ulifanikiwa, daktari wangu aliondoa kila uvimbe nikapona vizuri, lakini baada ya miaka mitatu uvimbe umerudi tena," amesema.





# CCM yaandaa vijana uchaguzi wa mitaa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeanza kutengeneza vijana maalum watakaobeba dhamana ya kutetea viti vyake vya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa 60 ya Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, isiangukie kwenye mikono ya wapinzani.

Vijana 300 walioibuliwa katika kila mitaa, waliwekwa kambini kwa siku tano kupigwa msasa wa namna watakavyokabiliana na hoja za wapinzani na kushinda uchaguzi ujao wa mitaa, vijiji na vitongoji, unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba mwaka huu.

Jana, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana (UVCCM) Wilaya ya Moshi Mjini, Sadath Ndibalema, alisema vijana hao wamepewa mafunzo mbalimbali yakiwemo ya ukakamavu, uzalendo, kutetea chama hicho na kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi huo.

Alisema kambi hiyo iliwekwa katika Chuo cha Maendeleo cha Singa, kilichopo Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Vijana hawa wamepata mafunzo ya aina nyingi, wamefundishwa uzalendo, kutetea chama chao na kusimamia misingi ya sheria taratibu na kanuni za nchi katika kuelekea kwenye chaguzi, lengo ni kupata viongozi bora na wenye tija kwa jamii yetu watakaoleta tija," alisema Ndibalema.

Akifunga mafunzo hayo, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, aliwataka vijana kuzingatia muda kwenye kila jambo huku akisisitiza kutoridhishwa na taaluma zao.

"Vijana, punguzeni kupoteza muda kwa mambo yasiyo na tija na kisha kujiita wasomi, ili uwe msomi mwenye tija ni lazima uweze kutafsiri ulichosoma kwa vitendo na kilete tija.

"Vijana wengi mnalalamika hakuna ajira lakini nyinyi hamjitumi kuwa wabunifu katika kutatua matatizo ya jamii na pia wengi wenu sio waaminifu, hii inafanya vijana kutoaminiwa kwenye kila eneo wanalofanya kazi.. hii sio dalili nzuri kwa kizazi kijacho mnapaswa kujitathmini" alisema Boisafi.

Naye Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Kilimanjaro, Ivan Moshi, alisema watu ambao watakifanya chama kushinda kwa urahisi katika uchaguzi mkuu wa 2025 ni viongozi wa dola waliochaguliwa mwaka 2020.

Alisema baadhi ya madiwani wamekuwa hawafanyi mikutano ya hadhara ya Wananchi lakini wamekuwa wakisuguana na Wabunge, ambapo kila mmoja amekuwa akimtupia lawama mwenzake na kukiomba chama kuhakikisha kila kiongozi anatimiza wajibu wake.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Zephania Sumaye, alisema CCM kinahitaji vijana jeuri na wenye akili ya kuhoji jambo na kuweza kulitetea mbele ya jamii.

Sumaye alisema kesho ya Tanzania imewekwa katika mabega ya vijana na sio rasilimali zilizopo ambapo kambi hizo zinasaidia vijana kupata elimu na kuwavija na vijana wenye uwezo wa kuhoji na kutambua mambo mbalimbali ya chama.

# Lema asema utalii chachu ya kumaliza tatizo la ajira

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MBUNGE wa zamani wa Arusha, Godbless Lema, amesema sekta ya utalii nchini ikitumika vizuri kama inavyofanya Morocco, Tanzania inaweza kutatua tatizo la ajira kwa vijana.

Akizungumzia tatizo hilo la ajira jana jijini Arusha, alisema kama nchi ikijiimarisha kwenye sekta ya utalii peke yake, Tanzania itaondokana na malalamiko yasiyokwisha ya vijana kukosa ajira.

"Nchi hii ikiweza kufanya matangazo ya utalii peke yake vizuri, na tukafika mbali. Morocco wanapokea watalii 700 mpaka 800 kwa mwaka. Utalii wao ni nyumba za kale na beach (fukwe).

"Lakini Tanzania wana mbuga zote za wanyama, wana Mlima Kilimanjaro, wana Hifadhi za Taifa, wana Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), wana mapori, wana beach zaidi ya sita, wanapokea zaidi ya watalii 600,000 kwa mwaka."

Kwa mujibu wa Lema, ukipokea watalii milioni 10 kwa mwaka, maana yake utaajiri watu milioni 20 mpaka 30; na ukitoa ajira milioni 20, ajira zitakuwa ni nyingi kuliko wananchi, kwa sababu Tanzania ina watu milioni 64.

"Sasa ukichukua total (jumla) ya milioni 20 ama 25, ukachukua waliobaki ni kama milioni 30. Ukachukua ajira milioni 20 kwenye utalii peke yake, maana yake hakuna dada angeitwa mama ntilie, kijana angeitwa bodaboda,"alieleza Lema.

Wakati Lema akisema hayo, Waziri wa Maliasili na Utalii Angelah Kairuki, wakati wa hafla ya kutangaza matokeo ya sensa ya wanyamapori na kuzindua ripoti ya taarifa ya watalii waliotembelea nchini mwaka 2023, alinukuliwa akieleza,

Idadi ya watalii imeongezeka kutoka milioni 1.4 mwaka 2022 hadi milioni 1.8 kwa mwaka 2023, huku ongezeka hilo likitajwa kuwa ni matokeo ya 'Filamu ya Royal Tour' ambayo iliongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan katika juhudi za kutangaza utalii nchini.

Vilevile, kiwango cha ujio wa watalii nchini kimefikia asilimia 118 kwa mwaka 2023, ikiwa ni ongezeka la asilimia 32 kabla ya ugonjwa wa Uviko 19.



Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa mwaka 2024, Geofrey Mnzava (katikati), akizindua mradi wa maji wa Bwagamoyo Kibaya wenye thamani ya sh. milioni 422 unaonufaisha watu 2,960, wilayani Kiteto, mkoani Manyara juzi. Kushoto ni Mbunge wa jimbo la Kiteto, Edward Ole Lekaita (kushoto), Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA) wa mkoa huo, Walter Kirita (wa pili kushoto) na Mkuu wa wilaya hiyo, Remidius Mwema. **PICHA: GIFT THADEY**

# Halmashauri yaomba mil. 65/ kumalizia ujenzi wa shule ya wasichana Machame

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

KUSUASUA kwa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Machame, kumeisukuma Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Kilimanjaro, kuiomba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sh. milioni 65 kumalizia mradi huo.

Ujenzi wa miundombinu hiyo umehojiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), akisema utaongeza gharama kubwa kwa serikali.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dionis Myinga, wamelazimika kuiandikia barua TAMISEMI ili kupata fedha za ziada za kuwezesha kukamilika mradi huo.

CAG alitoa mapendekezo sita kuhusu hoja ya kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya shule hiyo, iliyopewa na serikali Sh. milioni 372.6.

"Menejimenti imefanya ufuatiliaji wa karibu na kuweka juhudi zaidi katika kusimamia mradi huo ili kuhakikisha kuwa shughuli zilizobaki zinakamilika bila kuchelewa na kupata thamani ya fedha, ambapo bweni moja, vyumba vinne vya madarasa na vyoo matundu sita vimekamilika," alisema Myinga.

Mapendekezo ya CAG ni pamoja na kutaka kuharakisha utekelezaji wa shughuli za mradi ili kuepusha uwezekano wa kuongezeka kwa gharama kwa jumla ya fedha zilizotolewa.

Kuongeza juhudi katika kusimamia miradi inayotekelezwa, kwa lengo la kupata thamani ya fedha kwa miradi iliyo ndani ya Halmashauri mara fedha zinapotolewa.

Pendekezo lingine ni kuanzishwa mawasiliano na mamlaka inayohusika, ili kushughulikia uwezekano wa kuongezeka kwa gharama zaidi ya matarajio ya awali, ili kupata fedha za ziada kwa ajili ya kukamilisha shughuli za mradi.

Limo pia pendekezo la kutaka kuhakikisha mambo yanayosababisha kuongezeka kwa gharama yanazingatiwa na mamlaka, wakati wa utoaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya baadaye.

CAG pia alipendekeza kuanzishwa njia za wazi za mawasiliano na mafundi jamii, ili kuhakikisha kwamba wanafahamishwa kuhusu hitaji la kuomba kuongezewa muda, iwapo kuna ucheleweshaji wa mradi, na kutoa maoni ya kurefusha mara moja ili kuepusha usumbufu na migogoro isiyo ya lazima ya mradi.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Kifo 'tata' cha Zengekala kilivyoishtua Bongo

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni saa tatu usiku ya Desemba 17, 1987, kwenye kipindi cha majira, ndipo mtangazaji alipowatangazia Watanzania kifo cha ghafla cha mwanamuziki maarufu sana wakati huo, Nico Zengekala.

Kilichotokea ni taharuki. Hakuna aliyeamini kuwa Nico, mwimbaji mwenye sauti tamu, nyororo ambaye ni mlemavu wa macho, amefariki. Mwanamuziki ambaye tayari alikuwa ameshajinyakulia mashabiki wengi nchini Tanzania, miaka michache tu tangu aingie nchini kutokana na umahiri wake wa kuimba, akitokea kwao Kenya.

Habari zaidi zinasema kuwa hadi saa sita usiku, kuamkia kifo chake alikuwa anapiga soga na marafiki zake mitaa ya nyumbani kwake, Kariakoo mtaa wa Sikukuu, Dar es Salaam ambako alipewa nyumba ya kuishi na bendi aliyokuwa anapigia ya Juwata Jazz, wana Msondo Ngoma.

Zilikuwa ni moja kati ya nyumba zinazomilikiwa na Juwata.

Itakapofika Desemba 17 mwaka huu, Afrika Mashariki, itatimiza miaka 37 tangu ilipompoteza mwimbaji kijana, aliyefariki ghafla alfajiri saa 11 afajiri, nyumbani kwake ghafla Mtaa wa Sikukuu, Dar es Salaam kwa kile madaktari walichosema kuwa ni ugonjwa wa kifafa. Alifariki akiwa na umri miaka 24 tu.

Kutokana na ustaa wake, na kifo chake cha ghafla, ilisababisha taharuki kubwa, vilio, simanzi, na kila aina ya huzuni ilitawala, Tanzania, Kenya na Uganda, huku baadhi ya Wabongo wakiwa hawaamini kama kilikuwa ni kifo cha kawaida.

Ni kifo kilichozua maneno mengi kuliko kawaida. Wengine wakasema ni mambo ya kishirikina. Wapo waliodai alilishwa sumu. Na wengine walisema umaarufu wake alioupata kwa muda mfupi tu, ulikuwa ni mwiba kwa wanamuziki si wa Msondo tu, bali hata wa Tanzania nzima, alioneka kuwafunika, hivyo baadhi yao hawakupendezewa. Lakini yote hayo yanamalizwa na ripoti ya madaktari kuwa alifariki kwa ugonjwa wa kifafa.

Alipoingia nchini na bendi ya Les Cubano, alitamba na vibao kama 'Jackie', 'Mwalimu Nyerere', 'Suzzy', 'Bwana Salim', 'Shemango', 'Mama Hisani' na nyingine nyingi.

Mwaka 1985 alichukuliwa na Msondo ngoma ambako nako alitamba na vibao kama 'Solemba' alichokitunga mwenyewe na vingine akiviimba kwa ustadi mkubwa kama 'Hasira Hasara', 'Kaka Mahmood', 'Asha Mwanasefu', 'Prisila', 'Kambarage Nyerere' na nyingine.

Wengi hawajui kuwa Nico Zengekala aliimba kwa umahiri mkubwa na kutunga nyimbo ambazo hadi anafariki alikuwa hajazirekodi. Nazo ni 'Dalila', huku akitunga 'Cha Mlevi hulikuwa na Mgema', pamoja na 'Razole' ambazo kama angebahatika kurekodi ingekuwa habari nyingine.

Wimbo wa 'Tabu Mpaka Lini' ambao umerekodiwa, kuna baadhi ya vipande aliimba Nico, na alipofariki wakati wa kurekodi viliimbwa na watu wengine. Ni kile kilichoimbwa na Suleiman Mbwembwe "Bwana eee, ooh bwana ee, tabu hii mpaka lini jamani.", na kingine alichoimba Tino Masinge "Sikia eee, makosa tuliyoyafanya awali we mama tukifanya tena marafiki watatucheka." Hivi vyote awali ilikuwa virekodiwe na Nico, lakini alifariki kabla ya kwenda studio.

Alikuwa na sauti tamu, nyororo, kali, ambayo alikuwa na uwezo wa kuitetemesha na kusikika kama maporomoko ya maji, wakati mwingine akiishusha sauti kama mtu anayeweseka hivi.

Alizaliwa katika kijiji cha Wundayi eneo la Mwatate karibu na mji wa Voi, kilometa kiasi cha 100 hivi kutoka Mombasa nchini Kenya.

Alichukuliwa na kuletwa nchini na mabaki wa wanamuziki wa Super Volcano ya Mbaraka Mwinshehe aliyefariki Kenya mwaka 1979, Simba Wanyika, Les Wanyika, Wanyika Stars, Super Wanyika na Jobiso, ambao walimuona akiimba kwenye bendi moja ya Wataita wenzake Nairobi.

Wanamuziki hao ambao ni Watanzania waliokuwa nchini humo wakiendelea na shughuli za muziki, waliombwa kurejea nchini na Mkuu wa Mkoa wa Morogoro wakati huo Nicodemus Banduka, hivyo wakaamua kumchukua Nico, ambapo yeye mwenyewe pia alitaka kuondoka Kenya.

Kwa mujibu wa mwanamuziki Said Makelele ni kwamba ilibidi kwenda kumuomba baba yake, ambaye aliwakubalia kwa madai kijana wake ameshindikana, kwani amemkataza sana mambo ya muziki, lakini amekuwa akitoroka nyumbani na kwenda kuimba sehemu mbalimbali.

Makelele anasemailibidi wadanganye ni Mtanzania ili aruhusiwe kuvuka mpaka wa Tanzania na Kenya, kwani wakati huo alikuwa na umri wa miaka 17, hivyo asingeweza kuruhusiwa kuvuka. Wakadai ni Mtanzania wa Dodoma na wao ni wanamuziki wanaorejea nyumbani Tanzania kwa wito wa Mkuu wa mkoa wa Morogoro, ndipo waliporuhusiwa.




Aliyekuwa mwanamuziki na mwimbaji wa bendi ya Juwata Jazz, 'Msondo Ngoma', Nico Zengekala

Inawezekana wakati anafariki huenda alikuwa hajafikisha miaka 24, na inawezekana Msondo walimpandisha umri ili aweze kuajiriwa na Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania JUWATA, kwani wasingeweza kumuajiri mtoto.

Ni kwa sababu kama aliingia nchini ana miaka 17 na hakudumu na bendi hiyo kwa zaidi ya miaka miwili akajiunga na Msondo.

Ni mwanamuziki aliyedumu kwa muda mfupi nchini, lakini sauti na uimbaji wake hadi leo hi umeendelea kuwa lulu na wimbo wake wa 'Solemba' na msamiati ukiendelea kuishi.

Hakuwa staa kwao Kenya, lakini nyota ilimuwakia nchini na hata mwili wake uliposafirishwa, ulikuwa ni msafara na heshima kubwa wa magari lukuki ya serikali ya Tanzania, Jumuiya ya Wafanyakazi wa Tanzania, Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (Chamudata), wapenzi na mashabiki kama vile anayekwenda kuzikwa ni kiongozi mkubwa wa kitaifa.

Hii iliwashangaza kuwashangaza na kuwaliza wengi kwao, zaidi wazazi na ndugu zake, kwani aliondoka akiwa wa kawaida tu, lakini maiti yake imerudishwa nyumbani kishujaa. Hawakuamini.

Alizikwa kijiji kwao Wundayi, Mwatate, Voi, Taveta nchini Kenya Desemba 24, 1987.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Trump atangaza kuwafukuza wahamiaji akishinda urais

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump, amekubali rasmi uteuzi wa kuwania urais kwa tiketi ya Chama cha Republican katika mkutano mkuu wa chama hicho.

Katika hotuba yake ya dakika 90, Trump alitoa ahadi mbalimbali kwa Wamarekani ikiwa ni pamoja na kumaliza migogoro ya kimataifa na kutekeleza operesheni kubwa ya kuwatimua wahamiaji ambayo haijawahi kutokea katika historia ya Marekani.

"Nitamaliza kila mzozo wa kimataifa ambao umeanzishwa na utawala wa sasa, ikiwa ni pamoja na vita vya kutisha kati ya Russia na Ukraine, ambavyo visingetokea kama ningekuwa rais. Vita vilivyosababishwa na shambulio dhidi ya Israel, ambalo lisingetokea kama ningekuwa rais." alisema mwanasiasa huyo wa Republican.

Hotuba ya Trump ya kukubali uteuzi, imeashiria kukamilika kwa mkutano mkuu wa kitaifa wa chama cha Republican ambao ulifanyika kwa siku nne.

Kiongozi huyo anajivunia mafanikio aliyopata ya kuaminiwa na wakereketwa wa chama hicho kwenye uchunguzi wa kura ya maoni tangu mdahalo na Rais Joe Biden uliofanyika mwezi uliopita.

Rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump amesema iwapo atakuwa rais tena, atawafukuza wageni kwa namna ambayo haijawahi kushuhudiwa katika historia ya nchi hiyo.

Trump, pia aliahidi kupunguza mfumuko wa bei na kukomesha uingiaji wa wahamiaji nchini humo na kuahidi kukamilisha ukuta utakaotenganisha Marekani na Mexico, ambako wahamiaji mara nyingi huingilia.

Alisema atakomesha uhamiaji mara moja siku ya kwanza kwa kufunga mpaka. Trump, ambaye alitumia zaidi ya saa moja kuwasilisha hotuba yake, ambayo alizungumza zaidi baada ya kusoma.

Katika hali ya kushangaza, hotuba hiyo ya Trump imekuwa ikizungumzwa hata katika majimbo yaliyo ngome za chama cha Democratic kama vile Minnesota na Virginia

Wakati Trump anazidi kujiimarisha kuingia katika Ikulu ya White House, Rais Joe Biden anakabiliwa na anguko kubwa la umaarufu wake na wasiwasi uliotanda ndani ya chama chake kuhusu afya yake.



Donald Trump

Kiongozi huyo mwenye umri wa miaka 81, anakabiliwa na shinikizo kutoka chama chake kujiengua kwenye ugombea kutokana na wasiwasi wa umri wake.

**DW**




Abiria wakiwa uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa OaHare mjini Chicago, nchini Marekani, baada ya kusitishwa kwa safari zote kutokana na matatizo ya mtandao jana. **PICHA: REUTERS**

# Tatizo la mtandao lasimamisha dunia

**WASHINGTON,** MAREKANI

MATAIFA mbalimbali duniani yameripotiwa kukabiliwa na hitilafu katika mifumo yake ya mawasiliano na teknolojia na kuathiri shughuli za kawaida kwenye benki, viwanja vya ndege, sekta za habari na usafiri wa reli.

Nchini Marekani, kampuni kubwa za ndege zilisitisha huduma zake kutokana na tatizo la mawasiliano, hali kama hiyo iliripotiwa nchini Ujerumani na India.

Kampuni ya Microsoft inayomiliki teknolojia hiyo ilisema imechukua hatua kufuatia changamoto hiyo.

Katika taifa la Uingereza, kampuni kubwa inayoendeleza shughuli za reli ilipata matatizo ya mawasiliano katika mfumo wake wa IT.

Nchini Hispania viwanja vyake vyote vya ndege vilikabiliwa na tatizo hilo la mawasiliano. Kampuni tatu za usafiri wa angani nchini India, pia ziliripoti kupata changamoto katika mfumo wake wa kununua tiketi za usafiri.

**RFI**

# Jiji la Tel Aviv lashambuliwa, mifumo ya Israel yashindwa

**TEL AVIV, Israel**

MLIPUKO umetokea katika jiji la Tel Aviv nchini Israel usiku wa kuamkia jana na kusababisha kifo cha mtu mmoja na wengine wawili wamejeruhiwa.

Shambulizi hilo lililofanywa kwa njia ya anga mwendo wa 9:15 usiku, limesababisha taharuki kwa wakazi wa mji huo mkuu wa Israel.

Kulingana na jeshi la Israel, shambulio hilo lilitekelezwa na ndege kubwa isiyo na rubani ambayo inaweza kusafiri umbali mrefu.

Jeshi hilo lilisema jana asubuhi, mlipuko huo ulisababisha kifo cha mtu mmoja na wengine kadhaa kujeruhiwa.

Katika taarifa yake ilisema ndege hiyo isiyo na rubani iligunduliwa na jeshi la Israel lakini kosa la kibinadamu lilisababisha mifumo ya kuona adui na ulinzi kutofanya kazi.

Shambulio hilo limetokea baada ya miezi tisa tangu kuibuka vita kati ya Israel na wanamgambo wa Hamas.

Hata hivyo, waasi wa Houthi wa Yemen walidai kuhusika na shambulio hilo katika taarifa iliyotolewa jana.

Waasi hao walisema walitekeleza shambulizi hilo kwa kutumia ndege isiyo na rubani.

"Kikosi cha anga cha ndege zisizo na rubani ndani ya jeshi la Yemen kilifanya operesheni ya hali ya juu ya kijeshi, kikilenga moja ya malengo muhimu katika eneo linalokaliwa la Jaffa, linalojulikana na Israel Tel Aviv", alisema msemaji wa kijeshi wa waasi wa Yemen Yahya Saree.

"Operesheni hiyo ilifanywa na ndege mpya isiyo na rubani iitwayo "Jaffa", yenye uwezo wa kupita mifumo ya kumuona adui na isiyoweza kutambulika na rada. Aliongeza kuwa operesheni hiyo imefanikisha malengo yake.

Waasi wa Houthi kwa miezi kadhaa wamekuwa wakifanya mashambulizi kwa meli zinazopitia Bahari ya Shamu na Ghuba ya Aden, wakidai kuonyesha mshikamano na Wapalestina.

Jumamosi iliyopita walionya kwamba hawatasita kupanua operesheni zao za kijeshi hadi uchokozi huo ufike mwisho.

Mkazi mmoja anayeishi katikati mwa mji wa Tel Aviv aliliambia shirika la habari la AFP kwamba aliamshwa na mlipuko mkubwa ambao ulitikisa kila kitu.

Aidha jeshi liliripoti kuwa "tukio hilo linachunguzwa kwa umakini na kwamba mlipuko huo ulisababishwa na kuanguka kwa kilipuzi kutoka angani kulingana na uchunguzi wa awali .

Hata hivyo, ilisisitiza kuongeza doria zake za anga ili kulinda anga ya taifa hilo.

Jeshi la polisi lilieleza kwamba vikosi vya polisi vimefika kwenye eneo la tukio na wapo kwenye ukaguzi kwa vitu vya kutiliwa shaka.

Aidha, lilitoa wito kwa wakazi wa jiji hilo kuheshimu maagizo ya usalama, na kuacha kukaribia au kugusa uchafu au vipande ambavyo vinaweza kuwa na vilipuzi.

# HABARI PICHA



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na mgeni wake, Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, katika ukumbi wa Ikulu Jijini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU**



Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi (katikati mwenye gauni la batiki), akiserebuka na wanafunzi na wafanyakazi wa Chuo Kikuu cha Katoliki Mbeya (CUoM), aliposhiriki kongamano la mwaka mmoja wa Chuo hicho. **PICHA: NEBART MSOKWA**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, akizungumza na watumishi na wananchi wa Kijiji cha Idodoma, Kibakwe mkoani Dodoma, jana ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi. **PICHA: LUSUNGU HELELA**



Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2024, Geofrey Mnzava (katikati) akizindua mradi wa maji wa Bagamoyo, Kibaya wilayani Kiteto wenye thamani ya Sh. milioni 422 unaonufaisha watu 2,960 juzi. Kushoto ni Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Manyara, Walter Kirita, na Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Remidius Mwema. **PICHA: GIFT THADEY**



Wadau kutoka sekta mbalimbali za Serikali na binafasi wakiwa katika kikao kazi cha wadau cha kukusanya maoni kuhusu Rasimu ya Mpango Kazi wa Taifa wa Masuala ya Jinsia na Mabadiliko ya Tabianchi jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-**22**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

Baada ya salamu, wakaanza kutaniana na baadaye akamwambia alichokuwa anamuitia.

“Ndugu yangu, mdogo wangu ambaye nilikwambia ni askari kitengo cha IT, amenisaidia huku na huku, kahangaika kwa kuwashirikisha wenzake, hatimaye wamegundua kuwa namba hizi ni kweli hazina majina ya watu waliosajili, lakini zimesajiliwa maeneo ya Tabata Bima.”

“Kule kule karibu na nyumba kwa marehemu mpenzi wangu?” “Ndiyo, halafu cha kushangaza na kufurahisha kwa upande wetu, ni kwamba zote nne zimesajiliwa sehemu moja.” Akajibu Dokta.

“Duh!” Akashangaa Kamal. “Halafu zimesajiliwa muda huo huo kwa wakala mmoja anaitwa Shida Mrosso.” Akasema akimtazana Kamal kwa natasamu halafu akaongeza. “Kaniambia hivi, unaweza kwenda na kumuuliza waliosajili pale walisajili kwa majina gani. Hawawezi kuongopa kwa sababu huwezi kusajili bila kitambulisho cha Nida.” “Nashukuru sana Dokta Shija kwa msaada wako unaoendelea kunipa wewe na mdugu yako afande.” “Usijali Kamal, nitakusaidia mpaka mwisho kwa sababu niliapa wakati tunafanya uchunguzi wa mwili wa mpenzi wako mara ya pili, nikajisemea moyoni kuwa kama ningemfahamu huyu kijana alinayesingiziwa mpenzi wake kuna vitu ningemsaidia, kwa sababu ukweli ni kwamba hajaua, na uthibitisho ni jinsi nguvu ya fedha ilivyotumika kufika ukweli kuwa ameuawa, ionekane amengua kwa presha, ndugu na watu walivyokataa, tukaingia sisi tukachunguza na kugundua kuwa ameuawa, halafu ikatumika tena nguvu ya pesa kumtafuta muuaji feki, huku wale halisi wakilindwa.”

“Nakuhakikishia Dokta ninakuamini na tutakuwa nawe pamoja. Kazi hii nitaifanya kesho, nitakwenda Tabata Bima kituoni ambapo umesema ndipo eneo lake lipo. Naweza kuifanya kazi hii, nitapata majina ya watu hao. Nadhani tukiyapata tutakuwa kwenye njia sahihi ya kuelekea kwa muuaji au wauaji.” “Swadakta, tena aliniuliza anaweza kufanya kazi hii, nikamwambia jamaa mwenye mienendo yake kama askari mpelelezi, kwa hiyo kwake kazi hii ndogo sana, akacheka.”

Alipomaliza Dokta na Kamal nao wakaangua vicheko.




****************************

“Naitwa afande Nico, nimekuja hapa kwa kazi moja ndogo ambayo naomba ulisaidie Jeshi la Polisi.” Akadanganya.

“Kazi gani hiyo afande?” Akauliza dada huyo kwa woga. “Hapana, usiniogope, polisi ni rafiki wa raia kama tu anatekeleza kile ambacho ameagizwa kufanya na kutii amri bila shuruti.” Akasema Kamal kwa sauti ambayo alidhani itamfanya dada yule asiwe na woga.

“Natumaini wewe ndiyo Shida Mrosso.” Kitendo cha jina lake kufahamika bila kuulizwa kulizidi kumfanya dada huyo kuingiwa woga. Na alizidi kuamini kuwa aliyesimama pale ni askari polisi, tena ni mpelelezi, kutokana na kulitambua jina lake bila kuuliza. Alijua kuwa jina hilo ndiyo lililosajiliwa na mtu akituma pesa ni lazima litokee hivyo. Lakini hapo ameajiri wasichana wawili na mvulana mmoja ambao huwa wanamsaidia. Lakini hakuna yoyote ambaye anayemfahamu kuwa yeye ndiye mwenyewe Shida Mrosso.

“Ndiyo mimi.” Akaitikia kwa sauti ya chini.

Baada ya kumtoa hofu kidogo na kumpoza, Kamal sasa alijua matakwa yake yatatekekezwa.

“Naomba unisaidie kitu kimoja. Naomba uniangalilie majina ya watu waliosajili namba hizi na tarehe hii.” Akasema huku akimkabidhi kikaratasi chenye namba nne ambazo ndiyo zile zilizotumika wao kutumiwa meseji za vitisho na marehemu Mariamu.

Dada yule alizichukua na akafungua mkoba, kabla ya kutoa daktari, ambapo alianza kupekua. “Kaa hapa.” Shida alimpa kiti Kamal, akakaa na kusubiri majina ya waliosajili namba zile.

Kazi ya kusajili namba sasa alimuacha binti mwingine aliyefika hapo baadaye na yeye akawa na kazi kusaka majina.

Nusu saa baadaye akamgeukia Kamal. “Hizi hapa, namba nne zilizosajiliwa kwa wakati mmoja siku hii, mbili ni za Uledi Mwinyimvua na Abbas Abdallah. zimesajiliwa kwa kupishana kiasi cha dakika 10 mpaka 15 hivi, na kwa bahati nzuri ni mimi ndiye niliyewasajilia.”

“Ahaa! Vizuri sana bibie. Walifika kwa pamoja?” “Mhh! Sidhani, ila alipofika tu Abbas, dakika mbili baadaye akafika Uledi ni kama walifuatana hivi, lakini kila mtu na njia yake.” Jibu hilo lilimfanya Kamal kutabasamu. Alijua hao walikuwa pamoja, ila walijifanya hawafahamiani na hata kufika hapo, waliambizana mmoja aanze. Kwa maana hiyo ni lazima usajili wao na laini haukuwa na heri.

“Walikuwa wanazungumza pamoja?” “Hapana, walionyesha kama hawafahamiani.” Jibu hilo wala halikunfanya Kamal kuondoa wazo kuwa ni kweli hawakuwa wanafahamiana. Aliona walijifanya hafahamiani kwa sababu za kiusalama.

**Nakuhakikishia Dokta ninakuamini na tutakuwa nawe pamoja. Kazi hii nitaifanya kesho, nitakwenda Tabata Bima kituoni ambapo umesema ndipo eneo lake lipo.**

“Okay ahsante sana, kama kutakuwa na lolote nitafika tena hapa ili nipate msaada.” Alisema Kamal na kumuachia noti ya shilingi elfu kumi. Shida hakuamini. Awali alikuwa mwoga hasa alipogundua kuwa anaongea askari, na alijua huenda mwisho wake ukawa ni kukamatwa.

“Unajua bibie, namba hizi zimetumia kwenye uhalifu na katika uchunguzi ikagundulika kuwa laini zilisajiliwa hapa. Kwa hiyo usiwe na hofu, hili litatusaidia sasa kuwasaka hawa wahalifu.” Kamal alimuondoa hofu dada yule kwani angeweza kuona jambo halijaisha na kwamba ipo siku anaweza kuja kukamatwa. Shida alishukuru, na pia alimshangaa askari yule kwa kumpa bakshishi ya pesa, pamoja na maneno ya faraja ambayo yalimpoza na kumuondoa hofu. Ucheshi wake pia ulimuacha hoi.

“Nashukuru afande, karibu tena.” Kamal akatabasamu na kumtazama binti yule. Kwa sababu alikuwa ameshapata kile alichokuwa akikitaka, akapata fursa ya kutazama sasa kwa makini. Alikuwa ni mrembo kiasi na umbile la kuvutia. “Nitarudi tena, lakini siyo kusaka laini ya mtu aliyekuja kusajili, au mimi mwenyewe kusajili. Na wala sitorudi kufanya kazi hii ya polisi, ila nitarudi kwa ajili ya kazi binafsi.”

Shida naye alitabasamu.”Kazi binafsi, yaani gani hiyo?” “Kazi ya kuuliza maswali laini na mepesi, hiyo magumu kama haya niliyokuuliza. “Tena moja naomba nikuulize leo.” “Enhe swali gani hilo?” Shida alionekana kusahau kama dakika chache zilizopita alikuwa kwenye hali ya wasiwasi na kutetemeka.

“Kwa nini uliitwa Shida?” “Wenyewe wazazi wangu alinipa, mama huyo, kabla hajanizaa alipitia shida sana.” “Okay! Ila kwa sasa unaonekana siyo shida tena, nashauri jina lako lingekuwa Raha!” Kamal alisababisha binti wa watu kuangua kicheko kikali kama kwamba alikuwa anaongea na mtu aliyemzoea kwa muda mrefu. “Afande wewe kumbe una maneno hivyo!!?” “Sasa mwenzako ndiyo lilikuwa jina langu utoto, niliitwa Maneno, ila baadaye nilipokuwa nililibadilisha, na wewe nakushauri uwe Raha.” Ilibidi Shida azidi kukauka kwa kicheko, na kuhitaji mkono wake ugonge kwenye mkono wa Kamal, naye akafanya hivyo. Kamal akamalizika kwa kumpigapiga mgongoni. Shida alijisikia raha na amani.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# COASTAL YATANGULIA Z'BAR

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kutoa ratiba ya michezo ya Ngao ya Jamii, kikosi cha timu ya Coastal Union tayari kipo visiwani Zanzibar kujiandaa na michezo hiyo.

Kwa mujibu wa ratiba ya TFF, Coastal Union watacheza na Azam FC, Agosti 8 kwenye uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar na mshindi wa mchezo huo atacheza na mshindi kati ya Simba na Yanga kwenye hatua ya fainali.

**Kwa sasa kikosi cha wachezaji wa timu Coastal kipo Zanzibar kikijifua kwa ajili ya mchezo huo na hiyo ni baada ya kuondolewa kwenye michuano ya Dar Port Kagame Cup.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Abbas El Sabri, amesema baada ya kufika tu Zanzibar wameanza mazoezi ya utimamu wa mwili nyakati za asubuhi na jioni wanafanya mazoezi ya mpira uwanjani.

"Tumepiga kambi Zanzibar, kwa sasa tunafanya mazoezi ya 'Gym' kuwaweka fiti wachezaji na baadaye uwanjani, tunaamini ni sehemu sahihi kwani hata mechi yetu ya Ngao ya Jamii itachezwa huku, Azam watafika na kutukuta sisi tumeshakuwa wenyeji," alisema Sabri.

Coastal, imeamua kwenda kuweka kambi Zanzibar siku chache baada ya kuondoshwa kwenye michuano ya Kombe la Dar Port Kagame Cup linalofanyika jijini Dar es Salaam, huku wapinzani wao Azam kwa sasa wapo nchini Morocco kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.

Wakati Azam FC, itautumia mchezo huo kama maandalizi ya Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Afrika, Coastal itakuwa inajiandaa kucheza Kombe la Shirikisho barani Afrika ambapo imepangwa kucheza dhidi ya Bravo do Maquis ya Angola katika mchezo unaotarajiwa kupigwa kati ya Agosti 16 na 18 huku mchezo wa marudio ukipangwa kuchezwa kati ya Agosti 23 na 25.

# 'Zigo la Euro' lafika tamati

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU chache baada ya kumalizika kwa michuano ya soka ya Ulaya 'Euro 2024' na kushuhudia Hispania ikitwaa ubingwa kwa kuifunga England mabao 2-1 kwenye mchezo wa fainali, hatimaye shindano la 'Zigo la euro' imetamatika jana.

Mashabiki mbalimbali wa soka wamefanikiwa kuibuka washindi kwenye kampeni hiyo na baadhi yao kupata nafasi ya kwenda kushuhudia baadhi ya michezo ya michuano hiyo iliyofanyika nchini Ujerumani.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Meneja wa wateja maalum wa kampuni ya tigo, Mary Rutta, alisema kumalizika kwa shindano hilo ni nafasi nyingine ya kuanzisha kitu kingine kwa ajili ya wateja wake.

"Tumefanikiwa kupata washindi 47 ambao wamejishindia zawadi mbalimbali wakati wa fainali ya 'Euro 2024', kati ya hao washindi saba waliweza kwenda kushuhudia baadhi ya michezo katika fainali hizo, kwa sasa tumefikia mwisho," alisema Mary.

Mmoja wa washindi wa mwisho, Ibrahim John, alisema kwake amejisikia vizuri kuibuka mshindikwenye siku za mwisho za shindano hilo.

"Kwa kweli nashukuru, sikuwa na amini lakini baada ya kupigiwa simu nimeshinda, nimeamini na nimejisikia furaha sana, mashindano yamemalizika lakini nimepata kitu cha kukumbuka 'euro 2024'," alisema John.




Meneja wa wateja maalumu wa Tigo, Mary Ruta, akizungumza na waandishi habari (hawapo pichani) wakati wa kuhitimisha shindano la 'Zigo la Euro 2024' jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara yaiagiza BMT 'kuvibana' vyama vya michezo maandalizi

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imeliagiza Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kuvibana vyama vya michezo kuhakikisha vinawasilisha mipango yao kwa ajili ya kujiandaa na michezo ya Olimpiki ya mwaka 2028 itakayofanyika nchini Marekani.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana kwenye hafla ya kuiga na kuikabidhi bendera ya taifa timu ya taifa inayokwenda kwenye michezo ya Olimpiki ya mwaka huu nchini Ufaransa, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Sulemani Serera, alisema lengo la maagizo hayo ni kuhakikisha idadi ya washiriki wa michezo hiyo inaongezeka kwa ajili ya kuipeperusha vema bendera ya Taifa kupitia michezo.

"Mwaka huu tunawakilishwa na wachezaji saba tu, lengo letu ni kuona mwaka 2028 tunapeleka idadi kubwa ya wachezaji na Serikali itaendelea kushirikiana na vyama na mashirikisho ya michezo ili kufikia malengo ya kufanya vizuri, alisema Serera.

Kwa upande wake Rais wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Gulam Abdullah Rashid, alisema ili kupata nafasi ya kushiriki michezo hiyo lazima mchezaji afikie viwango vinavyohitajika na Olimpiki.

"Hatupeleki mchezaji ambaye hajakidhi vigezo vya kushiriki Olimpiki, hawa wote wanaokwenda ni wale ambao wamekidhi vigezo," alisema Rashid.

Aidha, Katibu Mkuu TOC, Filbert Bayi, alisema kuwa maandalizi ya safari hiyo yamekamilika ikiwa pamoja na kupata viza na tiketi kwa ajili ya kusafiria kwa wachezaji wote pamoja na viongozi.

Katibu huyo alisema timu hiyo itaondoka kwa makundi ambapo kundi la kwanza litaondoka Julai 22, kundi la pili litakalojumuisha waogeleaji litaondoka Julai 23 na kundi la mwisho litaondoka Julai 27 likiwa na wanariadha.

Makamu Mwenyekiti wa TOC, Henry Tandau amesema anaimani wachezaji hao watafanya vizuri kutokana na maandalizi waliyofanya.

## ZISIKUPITE

### MCTOMINAY ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inalenga kuipiku Fulham kupata saini ya kiungo wa kati wa Manchester United na Scotland, Scott McTominay mwenye umri wa miaka 27. ***(Sun)***

### ARSENAL KUJITOA KWA GUEHI

ARSENAL inatazamia kusitisha nia yao ya kumnunua mlinzi wa England, Marc Guehi huku Crystal Palace wakihitaji zaidi ya pauni milioni 70 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Englans mwenye umri wa miaka 24. ***(Mirror)***

### IVAN TONEY SASA BEI CHEE

KLABU ya Brentford inatarajiwa kupunguza gharama ya mshambuliaji wa England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 28 hadi chini ya pauni milioni 50 baada ya kukosa ofa kutoka kwa klabu nyingine. ***(Sun)***

### UNITED YAMGANDA UGARTE

MANCHESTER United bado inavutiwa na kiungo wa Paris St-Germain kutoka Uruguay, Manuel Ugarte mwenye umri wa miaka 23. ***(Sky Sports)***

### DAVID AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imekuwa ikiwasiliana na wawakilishi wa mshambuliaji wa Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24, kabla ya kuwasilisha ofa kwa Lille. ***(Football Insider)***

### QPR YAVUTIWA NA SINGH

KLABU ya QPR inavutiwa na winga wa zamani wa Bayern Munich, Sarpreet Singh mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### CALAFIORI AOMBWA

MLINZI wa Italia, Riccardo Calafiori mwenye umri wa miaka 22 ameombwa kushiriki katika maandalizi ya msimu mpya wa Bologna huku Arsenal ikijaribu kufikia makubaliano juu ya thamani yake. ***(Evening Standard)***

### ELYNE WAHI ATAKIWA LENS

CHELSEA imeripotiwa kuwasiliana na klabu ya RC Lens kumsajili mshambuliaji, Elye Wahi mwenye umri wa miaka 21, baada ya The Blues hao kushindwa kumpata Mfaransa huyo msimu uliopita. ***(L'Equipe)***

### RODRIGUES ATUA LYON

KLABU ya Lyon imeripotiwa kuwa tayari kutangaza usajili wa mshambuliaji wa Southampton mwenye umri wa miaka 16, Alejandro Gomes Rodriguez baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa England chini ya umri wa miaka 16 kusaini mkataba wa miaka mitatu. ***(Fabrizio Romano)***

### RAMOS AWINDWA CHELSEA

CHELSEA imeripotiwa kuulizia kupatikana kwa mshambuliaji wa Ureno, Goncalo Ramos mwenye umri wa miaka 23 na mshambuliaji wa Ufaransa, Randal Kolo Muani (25) Paris St- Germain ili kuchukua nafasi ya mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku. ***(HITC)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RABIOT AACHANA NA JUVENTUS

**TURIN,** Italia

KLABU ya Juventus imeachana na mchezaji wake, Adrien Rabiot baada ya miaka mitano ya kuhudumu klabuni hapo.

**Rabiot si mchezaji wa Juventus tena baada ya Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo kuthibitisha kwamba mkataba wa mchezaji huyo umefikia tamati.**

### ●●● Mkurugenzi wa michezo wa klabu hiyo amethibitisha huku klabu za AC Milan na Real...

"Ningependa kumshukuru Rabiot ambaye mkataba wake ulimalizika Juni 30.Tunapenda kumtakia kila la kheri," alisema Giuntoli.

Rabiot anaondoka Juventus baada ya miaka mitano ambapo ametwaa taji la Ligi Kuu mwaka 2020 na makombe ya Ligi mawili.

Vyanzo mbalimbali nchini Italia vimeripoti kwamba klabu ya AC Milan na Real Madrid ni miongoni mwa timu zinazoiwania saini ya mchezaji huyo Mfaransa ambaye amekataa kuongeza mkataba mpya Juventus uliokuwa na thamani ya Euro milioni 7.5 kwa mwaka.

## HABARI MICHEZO



# ENGLAND YAMSUBIRIA GUARDIOLA MBADALA WA SOUTHGATE

**LONDON,** England

CHAMA cha soka cha England, FA, kinaweza kuwa tayari kusubiri kumpa nafasi Pep Guardiola kuwa kocha wa timu ya Taifa, kwa mujibu wa ripoti.

Gareth Southgate alitangaza kujiuzulu kama kocha wa England siku ya Jumanne, siku mbili baada ya kufungwa na Hispania katika fainali ya Euro 2024. Simba Watatu hao walisafiri kurejea kutoka Ujerumani wakiwa na medali za mshindi wa pili mkononi baada ya bao la dakika za lala salama la Mikel Oyarzabal kuamua fainali hiyo kali.

Orodha ya watu wanaotarajiwa kuchukua nafasi yake imesalia kuwa ndefu, huku Lee Carsley, bosi wa sasa wa wachezaji wasiozidi umri wa miaka 21, Graham Potter na Mauricio Pochettino wakiwa miongoni mwa majina yanayotajwa.

Hata hivyo, kocha wa Manchester City Guardiola pia yuko kwenye rada za England na huenda nchi hiyo ikawa tayari kufanya mambo kwa busara ili kumleta.

Gazeti la The Independent linaandika kuwa FA inatamani sana ustadi unaooneshwa na bosi wa City, hasa uwezo wake wa kushinda mataji. Inafikiriwa kuwa Guardiola anaweza kumuacha mwajiri wake wa sasa mwishoni mwa msimu ujao, huku mkataba wake ukitarajiwa kumalizika mwaka 2025.

FA bado wanataka kufanya uamuzi wa haraka, lakini wanaweza kumteua Carsley kama kocha wa muda huku wakisubiri kumjaribu Guardiola. Hatua hii inaweza kuonekana kuwa ya kawaida, kwani Southgate aliteuliwa kwa njia sawa, kabla ya kufurahia miaka minane ya kuinoa timu ya taifa.

# Grenwood atua Marseille

**MARSEILLE,** Ufaransa

KLABU ya Marseille imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood, klabu hiyo ya Ligue 1 imethibitisha.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba mpango huo una thamani ya pauni milioni 26.7 na inajumuisha nyongeza.

Greenwood hajaichezea United tangu kusimamishwa na klabu hiyo Januari 2022 baada ya kukamatwa kwa tuhuma za ubakaji na unyanyasaji, huku Polisi wa Greater Manchester wakithibitisha kuwepo kwa "picha na video za mitandao ya kijamii zilizotumwa na mwanamke akiripoti matukio ya ukatili wa kimwili."

Greenwood mwenye umri wa miaka 22, alitumia msimu uliopita kwa mkopo Getafe kule LaLiga, akifunga mabao nane na kutoa asisti sita.


Kocha wa Marseille, Roberto De Zerbi, ambaye aliihama klabu ya Ligi Kuu ya England ya Brighton baada ya msimu wa 2023-24, alisema wiki iliyopita kwamba hatakuwa na chuki dhidi ya Greenwood kwa sababu ya maisha yake ya nyuma.

"Mason ni mchezaji wa kiwango cha dunia, lakini bado hatujamsajili. Sijui nini kilitokea, lakini sijazoea kujihusisha na maisha ya faragha ya wachezaji wangu," alisema.

"Lakini akija hapa, lazima ujue kwamba ninawatendea wachezaji wangu wote kama wanangu.

Ninaweza kuwasema kwa faragha, lakini siwezi kuwashambulia hadharani."

Meya wa jiji hilo la Ufaransa pia alipima uzito kuhusu uhamisho huo wiki iliyopita, akitaja madai dhidi ya Greenwood kuwa "hayasemeki" na kuongeza kuwa atamwomba rais wa Marseille, Pablo Longoria kutomsajili mchezaji huyo.





# Man Utd yamtwaa rasmi Yoro

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER, United imekamilisha usajili wa mlinzi, Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18 kutoka Lille ya Ufaransa, klabu hizo mbili zimethibitisha.

United ilikubali ada ya euro milioni 62 pamoja na nyongeza, ili kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa chini ya miaka 21, vyanzo viliiambia ESPN.

Yoro amejiunga na United licha ya kutakiwa na Real Madrid, baada ya vyanzo kuiambia ESPN kwamba timu hiyo ya Hispania ilichagua kutojihusisha na vita ya kuwania nafasi ya kumsajili nyota huyo na klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

Vyanzo vya habari viliongeza kuwa Yoro aliiambia Madrid kuhusu nia yake ya kusaini United Jumanne usiku baada ya klabu hiyo ya Hispania kushindwa kufanya harakati za kumsajili.

"Kusaini kwa klabu yenye hadhi na matarajio ya Manchester United mapema sana katika maisha yangu ni heshima kubwa," alisema Yoro.

"Tangu mazungumzo yangu ya kwanza na klabu, waliweka mpango wazi wa jinsi ninavyoweza kujiendeleza huko Manchester kama sehemu ya mradi huu wa kusisimua, na walionesha kujali sana kwangu na familia yangu.

"Ninajua kuhusu historia ya wachezaji wachanga katika Manchester United na ninahisi inaweza kuwa mahali pazuri kufikia uwezo wangu na kufikia matarajio yangu, pamoja na wachezaji wenzangu wapya. Siwezi kusubiri kuanza," alisema Yoro.

Beki huyo ataungana na Joshua Zirkzee, aliyesajiliwa kutoka Bologna Jumapili, Old Trafford.

## HABARI MICHEZO

### Gamondi: Nguvu zetu kwenye ubingwa

INATOKA UKURASA 24

alisema michezo mitatu watakayoicheza nchini humo anaamini itamsaidia kocha Gamondi katika kuandaa timu yake kabla ya kurejea nchini kwa ajili ya ratiba nyingine.

"Kitakuwa kipimo kizuri kwetu, kucheza na timu kama Augsburg inayocheza Ligi Ujerumani ni kitu kizuri, kocha atapata muda wa kuangalia nini cha kuboresha, mechi tatu za Afrika Kusini itakuwa sehemu nzuri ya maandalizi yetu," alisema Hersi.

Yanga inatarajia kuwa na tamasha lake la kila mwaka 'Wiki ya Mwananchi' ambalo kilele chake kimepangwa kuwa Agosti 3 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam.

### Wachezaji Simba wapeana semina kuikabili Yanga

INATOKA UKURASA 24

nchini hivyo wanaelewa mazingira na nini wanatakiwa kufanya.

Beki huyo wa kushoto alisema mbali na mkakati huo kabambe kuhakikisha wanashinda mechi hiyo, lakini pia wako kwenye maandalizi ya Simba Day, pamoja na ya msimu mzima wa mashindano.

"Pamoja na hayo, pia akili yetu ipo kwenye maandalizi ya msimu mzima, kabla ya hapo tuna mechi ya kirafiki ya 'Simba ' ambayo itakuwa ni maadalizi tosha ya mchezo wa watani," alisema nahodha huyo.

Kwa upande wake, straika Freddy Michael aliyesajiliwa katikati ya dirisha dogo la usajili, amesema anajua nini wanataka mashabiki wa Simba hivyo amejipanga kufunga magoli mengi.

"Tuna wachezaji wazuri sana, na mazoezi yamekuwa 'sapraizi' sana kwetu, hasa mimi nimefurahi kwa kuanza mazoezi ya maandalizi nikiwa na timu hii tofauti na nilivyokuja, nataka nionyeshe nilichonacho kwenye ligi. Nitajitahidi kila njia ili kuisaidia timu na kuwaridhisha mashabiki wa Simba ambao wanataka mabao zaidi kutoka kwangu," alisema mchezaji huyo raia Ivory Coastal aliyesajiliwa kutoka Green Eagles ya Zambia.

Wakati huo huo, wachezaji Willy Onana na Awesu Awesu, wamewasili kwenye kambi ya timu hiyo nchini Misri.

Onana amerudishwa baada ya klabu hiyo kushindwa kupata saini ya Willy Mpanzu huku Awesu akiwa ni mchezaji mpya aliyesajiliwa kutoka KMC.

# KOCHA AZAM FC AKUNWA KAMBI MOROCCO, MISOSI

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA msaidizi wa Azam FC, Youssouph Dabo, ameonyesha kufurahishwa na mazingira ya kambi nchini Morocco, akisema imekuwa na vitu vingi chanya ikiwemo utulivu wa wachezaji wake, vifaa vya mazoezi, viwanja bora pamoja na vyakula.

Akizungumza akiwa nchini humo ambapo kikosi cha timu hiyo kimepiga kambi kwa maandalizi ya msimu ujao wa mashindano, ikiwemo Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara, Dabo amesema mazingira waliyoyakuta yamewafanya wao kama makocha kurahisishiwa kazi ya kuandaa kikosi bora na chenye ushindani.

"Tumepata kambi nzuri kwa maandalizi ya msimu, ni sehemu nzuri sana maana kila kitu kipo sehemu moja, ubora wa sehemu ya kuchezea ni wa viwango vya juu, vifaa vya mazoezi, hata vyakula, hii imetufanya hata makocha tusiwe na kazi kubwa sana ya kutengeneza ubora na utimamu wa mchezaji kwa sababu kila kitu kipo kwenye ubora wa hali ya juu," alisema.

**Alisema kabla ya kurejea nchini watapata mechi tatu za kirafiki ambazo wao kama benchi la ufundi watazitumia kupima kikosi chao kimefikia wapi kimaandalizi na baada ya hapo wataangalia ni kitu gani cha kuongeza.**

Kocha huyo pia amefurahishwa pia na usajili wa mchezaji Cheickna Diakite raia wa Mali aliyetokea klabu ya AS Real Bamako ya nchini humo.

Alisema usajili wa mchezaji huyo unataongeza ubora kwenye kikosi cha Azam FC kwa sababu anafahamu kijana huyo ana kipaji kikubwa.

"Ni mcheaji mzuri, tunampenda, tulihitaji mchezaji wa kiwango chake, huwa sichukui mchezaji ili mradi, bali mchezaji wa kutuongezea ubora, kama nitapata mwingine mzuri ninaweza kumsajili pia," alisema.

Diakite, anayecheza winga zote mbili amesajiliwa kuchukua nafasi ya Kipre Junior ambaye ametimkia MC Alger ya Algeria.




Wachezaji Shaban Mussa (kulia), na Idrisa Hessein wa Kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa kituo hicho jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kamara afurahishwa maandalizi Singida BS*

**Na Faustine Feliciane**

GOLIKIPA mpya wa klabu ya Singida Black Stars, Mohamed Kamara, amesema anafurahishwa na maandalizi ya timu hiyo kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania bara.

Kamara aliyesajiliwa hivi karibuni na klabu hiyo baada ya kuachana na klabu ya Horoya ya Guinnea, alisema kuwa ana matumaini ya kuisaidia timu yake kuweza kufanya vizuri kwenye Ligi.

Alisema kwa sasa yupo kambini na timu hiyo kujiandaa na taratibu anaanza kuzoea mazingira ya hapa nchini.

"Kwa sasa tupo Arusha kambini, japo huku kuna baridi lakini taratibu naanza kuzoea hali ya hewa, naamini baada ya muda kidogo nitakuwa vizuri zaidi, nafurahi kuwa hapa," alisema Kamara.

Aidha, alisema anafahamu ushindani uliopo kwenye ligi ya Tanzania na wao wanajiandaa vizuri kukabiliana na upinzani huo msimu ujao.

"Huu utakuwa msimu wangu wa kwanza kucheza hapa Tanzania, nafahamu ugumu wake, najua kuna timu nyingi nzuri na nyingine zina majina hata nje ya Tanzania, naamini tutafanya vizuri," alisema Kamara.

Singida Black Stars, tayari imeshaanza maandalizi kuelekea msimu ujao na kwa sasa wameweka kambi yao jijini Arusha.

# Michezo


Jumamosi Julai 20, 2024

Nipashe




Man Utd yamtwaa rasmi Yoro

UKURASA 22




Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi.

## Wachezaji Simba wapeana semina kuikabili Yanga

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa muda mrefu ndani ya kikosi cha Simba wameanza kuwapa semina elekezi wenzao wapya waliosajiliwa msimu huu juu ya utamaduni wa timu hiyo na na umuhimu wa mechi ya 'dabi' katika soka la Tanzania.

Nahodha wa kikosi hicho, Mohamed Hussein 'Tshabalala', amesema mara baada ya kufahamu tarehe na uwanja utakaochezwa mechi ya Ngao ya jamii dhidi ya watani zao Yanga, yeye na wachezaji wenzake waliopo kwenye kikosi hicho muda mrefu, wameanza kuongea na wenzao wapya hasa wale wa kigeni juu ya utamaduni wa mechi hiyo na umuhimu wa kushinda.

"Mechi dhidi ya watani tulikuwa tunaifahamu, ambacho hatukufahamu ni tarehe na uwanja tutakaocheza, sasa tumeshafahamu, kwa sasa tuna wachezaji wengi wapya hasa wa kigeni, tumeanza na tunaendelea kuwakumbusha umuhimu wa mechi hiyo, tunawaaambia katika nchi yetu mechi kubwa ni ya Simba na Yanga, ni dabi na ipo katika tarehe za mwanzo kabisa kabla ya msimu kuanza, tunawakumbusha kuwa ni muhimu kushinda mechi hiyo kwa sababu itawafanya hata wao kuwa na utulivu na kutokuwa na presha kutoka kwa mashabiki kama tukipata ushindi," alisema Tshabalala ambaye yeye na kikosi cha Simba wapo nchini Misri kwa ajili ya maandalizi ya mwanzo wa msimu.

Mechi hiyo ya Ngao ya Jamii, maalum kwa ajili ya kufungua msimu mpya wa Ligi Kuu, itachezwa Agosti 8 saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na mshindi atacheza fainali Agosti 11 dhidi ya mshindi kati ya Coastal Union au Azam FC, mechi hiyo itachezwa saa 10:00 jioni kabla ya mechi ya watani, Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar.

Simba inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa na idadi kubwa ya wachezaji wapya wa kigeni waliosajiliwa kutoka sehemu mbalimbali barani Afrika.

Pia itakuwa na wachezaji wapya wazawa ambao imewasajili kuelekea msimu mpya.

Tshabalala alisema shida ni ndogo kwa wazawa kwa kuwa wao wanafahamu mazingira na utamaduni wa mechi hiyo ambapo mbali na kwamba ndiyo kwanza watakuwa wanacheza dabi hiyo lakini wamezaliwa na kukua

ENDELEA UKURASA 23

# Gamondi: Nguvu kwenye ubingwa

**Na Faustine Feliciane**

## Kocha huyo haifikirii sana ngao ya jamii, mechi za Afrika Kusini kumpa...

SIKU chache baada ya Shirikisho la soka Tanzania (TFF) kutoa ratiba ya michezo ya Ngao ya Jamii itakayoanza Agosti 8, Kocha wa klabu ya Yanga, Miguel Gamondi, amesema akili yake ameielekeza kwenye kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kufanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa na haifikirii sana michezo ya Ngao ya Jamii.

Gamondi, ameyasema hayo muda mfupi kabla ya timu yake kuelekea Afrika Kusini kwenye mashindano maalum ambayo Yanga amealikwa.

**Alisema ameona ratiba ya michezo ya Ngao ya Jamii na anafahamu hamu ya mashabiki wa soka kuiona timu yake, lakini ameweka nguvu kwenye kuandaa timu kwa ajili ya ubingwa wa Ligi Kuu.**

"Tunataka kufanya vizuri zaidi kwenye mashindano ya kimataifa pia, tumeanza maandalizi yetu na tunaenda Afrika Kusini ambapo naamini tutapata maandalizi mazuri zaidi kuelekea kwenye msimu mpya, tutacheza michezo mitatu ambayo itakuwa kipimo kizuri kwetu," alisema Gamondi.

Aidha, alisema baada ya kambi hiyo ya Afrika Kusini watarejea kwa ajili ya tamasha la klabu hiyo la 'Wiki ya Wananchi' na baadae michezo ya Ngao ya Jamii.

"Kwangu sio kipaumbele sana Ngao ya Jamii, nguvu yetu kwenye ligi na michuano ya kimataifa, tunataka kujaribu kufika mbali zaidi kwenye mashindano ya CAF zaidi ya msimu uliopita," alisema Gamondi.

Kikosi cha Yanga tayari kipo Afrika Kusini kushiriki mashindano maalumu nchini humo ambapo leo wanatarajia kucheza na timu ya Augsburg kutoka Ujerumani.

Baada ya mchezo huo wa leo, Yanga itashuka tena uwanjani kucheza na TS Galaxy kabla ya kumaliza mashindano hayo kucheza na wenyeji wao, Kaizer Chief inayonolewa na kocha wa zamani wa Yanga, Nasreddine Nabi.

Rais wa Yanga, Hersi Said,

ENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >